SportPesa
TZS. 961,840,460
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Viwavijeshi** vyateketeza maelfu hekari za mazao

UKURASA 3


# Nipashe

Jumanne Februari 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580864

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**ARTETA: ODEGAARD ANAFAA KUWA NAHODHA**

UKURASA 22

# JK afichua sababu kumteua Dk. Mwele

UKURASA 2

• **Mamia** wajitokeza kwenye maziko yake...

*Endelea ukurasa 2*





Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete na mkewe, Mama Salma Kikwete, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti wa Magonjwa ya Kitropiki Yasiyopewa Kipaumbele wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Mwele Ntuli Malecela, baada ya mazishi yake, kijijini kwao, Mvumi, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, jana. **Picha ndogo:** Watoto wa marehemu, Naomi (kushoto) na Nenewa, wakiweka udongo kwenye kaburi la mama yao.

## Serikali kufungia mwandishi siyo chombo cha habari

UKURASA 2

RUFANI YA SABAYA

## Jamhuri: Zilitumika silaha kupora

UKURASA 3

**MICHEZO** ADEBAYOR KUVUNJIWA BENKI SIMBA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, Kilimo na Viwanda Tanzania (TCCIA), Mkoa wa Mara, Boniphace Ndengo (katikati), akizungumza wakati wa kikao cha kuhitimisha kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango inayoendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mjini Musoma, mkoani Mara jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo. **PICHA: TRA**

# JK afichua sababu kumteua Dk. Mwele

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, amefichua siri ya kumteua Dk. Mwele Malecela mwaka 2010, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Dk. Mwele alifariki dunia Februari 10, mwaka huu, kwa saratani ya kichwa nchini Uswisi akiwa anafanya kazi Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa nafasi ya Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele, Geneva Uswisi.

Akitoa salamu za pole kwa wanafamilia na mamia ya waombolezaji, alisema kilichomvutia ni ujasiri wake wa kuyasema magonjwa mbalimbali hususan matende na hakuwa na kigugumizi.

Alisema kuna wakati alimwambia huogopi kuyasemea na alimjibu ndiyo kazi yetu kusema na kwamba lazima kuyataja yalivyo.

"Aliendelea na kazi nilivyokuwa Rais nilimteua, nilimwita nikamwambia nataka nikuteue akasema nakushukuru sana kaka, nikamwambia naamini utaiweza akasema sina wasiwasi nitaimudu tu," alisema jana kwenye maziko yake Mvumi wilayani Chamwino, mkoani Dodoma na kuongeza:

"Kwa kweli amefanya kazi nzuri iliyotukuka, nakumbuka katika kipindi cha wimbi la kikombe cha Babu wa Loliondo alikuwa Mkurugenzi wa NIMR, watu wanakwenda, wanatoa wagonjwa hospitalini hata kwenye Baraza la Mawaziri niliona wanakunywa."

"Tulipitia kipindi kile kigumu vizuri alitushauri serikali, santuri ikaisha ugumu wake (kikombe), baadaye alipata kazi WHO Afrika na baadaye Makao Makuu...nilikutana na Mkurugenzi wa WHO namuuliza dada yangu anaendeleaje akaniambia ndiyo mkono wangu," alisema.

Kikwete alisema "Mzee John Malecela umepoteza mtoto, familia imepoteza mwanafamilia muhimu, mimi nimepoteza dada maana kila tukikutana namwita dada, rafiki, lakini taifa limepoteza mmoja wa raia wema, wazalendo wa kweli. Mwele ameondoka siyo rahisi kuamini kama hatunaye, hatutamwona na hatutakutana tena."

Alisema taifa litamkumbuka kwa mema mengi aliyoifanyia nchi na dunia kwa ujumla.

"Rais Mwinyi alikuwa anapenda kusema unataka historia yako iandikwaje nafikiri historia ya Dk. Mwele imeandikwa vizuri sana hivyo tunatakiwa kuungana kwa pamoja na familia kumwombea mapumziko mema na mzee tunakupa pole sana kwa msiba huu mzito," alisema Kikwete.

Aidha, Kikwete aliongoza viongozi wa serikali na mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa katika maziko.

Kikwete aliwasili katika kijiji cha Mvumi nyumbani kwa Waziri Mkuu mstaafu, Mzee John Samwel Malecela, majira ya saa 9:30 alasiri akiwa amefutana na mkewe Salma Kikwete na kupokelewa na viongozi wengine akiwamo Waziri Mkuu mstaafu wa awamu ya tatu, Fredrick Sumaye na wawakilishi kutoka (WHO).

Awali, katika ibada ya kuaga mwili wa Dk. Mwele, iliyofanyika katika Kanisa la Aglikana Dayosisi ya Kati, Askofu wa Kanisa hilo Dk. Dickson Chilongani, alisema hakuna msiba unaouma sana kama kuondokewa na mtoto wa kumzaa.

"Sote tunategemea sana kutangulia kabla ya watoto wetu, lakini Mungu ndiye amepanga na ikitokea hivyo hakuna anayeweza kuvumilia maumivu yake, maneno ya kibinadamu hayawezi kuondoa maumivu yenu Mungu ndiye pekee atakaye ondoa maumivu hayo.

"Dk. Mwele alikuwa na mchango mkubwa sana kitaifa na kimataifa tulitamani aendelee kuwapo ameondoka mapema sana wakati ambao bado tulikuwa tunahitaji kunufaika na matunda yake jambo la muhimu ni sisi kuendelea kuenzi mema yake aliyofanya katika wakati wa uhai wake,"alisema Askofu Dk. Chilongani.

Sumaye alisema: "Napenda kuungana nanyi katika msiba huu ...nitamkumbuka sana kwa jambo moja ambalo ni misimamo yake aliyokuwa nayo katika mambo ambayo yeye alikuwa anaamini hakuwa mtu wa kuyumbishwa na mtu katika kile anachokiamini."

Aidha, alisema Tanzania imempoteza mtu ambaye matunda yake yalikuwa bado yanahitajika kitaifa na kimataifa na taifa litaendelea kujivunia kazi aliyoifanya ndani na nje ya mipaka yake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Kazi Maalum Ikulu), George Mkuchika, alisema Dk. Mwele, alikuwa ni mcha Mungu.

"Mara nyingi tulikuwa tunakutana na Dk. Mwele baada ya kutoka kwenye ibada alikuwa anapenda sana kujiombea mwenyewe ndiyo maana hata leo hii sisi tunamwombea ni kazi sana kumwombea mtu ambaye alikuwa haombi wakati wa uhai wake," alisema Mkuchika katika maziko hayo yaliyohudhuriwa na umati.

## Serikali yalegeza makali kwa vyombo vya habari

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema itamfungia mwandishi atakayeandika habari yenye utata na si chombo cha habari kilichochapisha.

Akihojiwa na chombo kimoja cha habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema:

"Kwenye vyombo vya habari hasa upande wa 'print' (magazeti) hatuna mpango wa kufungiana, mpango wetu kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Mwaka 2016 ni kukushughulikia wewe uliyeleta shida."

Alisema kufungia gazeti ni sawa na kuwaadhibu wengine ambao hawahusiki na makosa ya mtu mmoja, huku akitolea mfano wa mfagiaji na 'vendor' (wakala) ambao hawahusiki kabisa na makosa ya kiuandishi.

"Gazeti lina wafanyakazi 50 yule mfagiaji, mhasibu, 'vendor' hausiki na 'story' (habari)...kuna mtu ameandika 'story' ya utata, halafu sisi tunakwenda kuwaadhibu wote mpaka ambao hawakuhusika, kichwani kidogo inakataa, mbona daktari akikosea hatufungi hospitali, tunamshughulikia yule daktari, "alisema na kuongeza:

"Ndiyo maana nikasema tutengeneze mazingira sheria hii itupeleke mahali ambako tutakupa leseni wewe mwandishi wa habari, ukikosea tukushughulikia wewe wengine waendelee kwa sababu hawahusiki na makosa yako," alifafanua.

Alisema kuwa pia Rais Samia Suluhu Hassan amewaambia wapitie sheria na kanuni za wizara zao, ili ziendane na wakati pamoja na mazingira ya sasa.

Pia alisema kuna mchakato unaoendelea kutunga sheria ya 'data protection', ili kuzuia uvujaji wa mazungumzo bila ridhaa ya wahusika, ikiwa ni s ehemu ya faragha za matumizi ya simu.

"Nadhani baadhi ya haya makosa yatashughulikiwa kwenye sheria tunazorekebisha, hata dunia inatuliza data zetu zipo salama kiasi gani, kwenye mchakato wa hizi sheria tunazozitunga ikiwamo ya 'data protection' tutashughulikia hilo ili watu wajiamini kuwa wapo huru na faragha zao zimelindwa,"alisema.

Pia alitoa rai kwa yeyote ambaye faragha yake katika mawasiliano itavujishwa atoe ripoti kwenye Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ili wahusika washtakiwe kwa kukiuka sheria.

Kama tumekuadhibu kwa sababu umeandika story (habari) mbaya halafu ukaiweka kwenye gazeti na online (mtandaoni).

Kuhusu Bunge mubashara (live) Waziri Nape, alisema kuwa uamuzi huo haukuwa wa serikali bali wa Bunge lenyewe ingawa serikali ndiyo iliyotoa amri ya kuondoa mubashara huo.

"Kwa sababu serikali ndiyo ilikuwa mstari wa mbele, tuliwaondoa TBC na wengine, lakini napenda nirudie kwa msisitizo sana kwamba matangazo ya bunge ni suala la Bunge lenyewe," alisema.

Alisema kuwa ni matumaini yake kuwa wataboresha namna Bunge linavyopaswa kuendeshwa na yupo tayari kushirikiana na muhimili huo, ikiwa kutakuwa na kanuni itakayoonyesha matangazo yanarushwaje.

"Kanuni za kuendesha vipindi vya Bunge ndizo zitakazosema, vipindi gani vinakwenda 'live', kwa staili gani? Kwa namna gani? Nani anavirusha? Anayevirusha analipwa au analilipa Bunge?" Alifafanua.

## HABARI KITAIFA

RUFANI YA SABAYA

# Jamhuri: silaha zilitumika kupora mali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKILI wa wajibu rufani kwenye kesi ya jinai namba 105, Ofmedy Mtenga, amedai mahakamani kuwa silaha zilitumika katika tukio la kupora fedha na mali nyingine katika tukio linalodaiwa kufanywa na Lengai Ole Sabaya kwenye duka la Mohamed Saad, lililoko Mtaa wa Bondeni jijini Arusha.

Wakili huyo alitoa madai hayo jana wakati wa usikilizwaji wa Rufani namba 129, katika shauri lililokuwa linamkabili, Ole Sabaya na wenzake wawili, mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Sedekia Kisanya.

Akijibu hoja ya saba ya mawakili wa waleta kwa nini wateja wao walistahili kutiwa hatiani na kufungwa miaka 30 kwenda jela, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mtenga, alidai kwamba kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa na mashahidi wa mashtaka katika tukio hilo kulikuwapo na silaha.

Alidai kwamba kwa mujibu wa shahidi wa sita wa mashtaka Bakari Msangi, kwenye kielelezo cha kwanza walichokitoa mahakamani cha maelezo aliyoandika Kituo Kikuu cha Polisi Arusha, silaha zinaonekana kutumika katika tukio la kupora mali na kuwaweka watu chini ya ulinzi.

"Ushahidi unaonyesha kuwa kulikuwapo na watu wengi siyo rahisi kwa kila mtu kuona kila kitu kinachoendelea kwa kuwa kila mmoja alikuwa amewekwa kwenye sehemu yake, pia siyo kila mmoja atakuwa jasiri wa kuangalia tukio linavyoendelea."

"Mazingira ya tukio yalikuwa mabaya sana hivyo kwa mashahidi kujichanganya kwenye maelezo yao, ni kutokana na wao kuwa sehemu tofauti na wengine wakiwa wamelazwa kifudifudi na kufungwa pingu, Wakili Mtenga,"alidai.

Naye Wakili wa Serikali, Veridiana Mlenza, alipinga hoja ya kwamba aliyeandikwa kwenye hati ya mashtaka, Mohamed Saad ni tofauti na yule aliyekwenda mahakamani kutoa ushahidi, Mohamed Saad Hajirini.

"Jaji hoja yao haina mashiko kilichotokea ni kwamba katika hati ya mashtaka yalitumika majina mawili na shahidi alipokuja hapa mahakamani alijitambulisha kwa majina matatu hivyo hakuna utofauti wa majina kama walivyodai kwa kuwa eneo ni sahihi na halina utata wowote," alidai Mlenza.

Alidai ya kuwapo kwa mkanganyiko eneo la tukio lilipotokea na duka lilipo haina msingi kwa kuwa ni sehemu sahihi na waleta rufani awali walikaa kimya.

Naye Wakili Mwandamizi, Baraka Mgaya, alidai kuhusu kufanya marekebisho ya hati ya mashtaka kwa kuwa kuna vitu ambavyo havikuorodheshwa, ikiwamo waleti kwenye eneo hilo, aliwezi kuathiri chochote kwa kuwa shahidi wa sita wa mashtaka, Bakari Msangi, alikana kuwapo na pochi siku ya tukio.

Aliieleza Mahakama kwamba kwa mujibu wa shtaka la tatu, fedha na simu aina ya Tekno Pop 1 ziliorodheshwa katika hati ya mashtaka isipokuwa karatasi ya mahitaji, ambayo waliona haina thamani na wasingeweza kuthibitisha mahakamani.



"Kushindwa kuthibitisha kitu kimoja haiwezi kufuta kabisa shtaka hilo na katika shtaka la kwanza kuna vitu viwili viliongezeka vikiwamo fedha za sarafu na mashine ya kielekroniki na kwa mujibu shahidi wa pili washtaka, alidai kwamba hakufahamu kiasi hali cha sarafu, lakini kwa suala la EFD ni mali na ombi letu wakati Mahakama yako ikitoa uamuzi iangalie kwa kosa la kwanza kutokuwekwa kwa mashine hiyo, je, iliwaathiri nini waleta rufani?"

Wakili Mlenza alidai kwamba hati hiyo siyo batili na imekidhi vigezo vya kisheria na warufani walifahamu ni makosa gani yanawakabili.

Vile vile, Wakili Mtenga alidai hakuna utata katika suala la utambuzi wa mleta rufani wa tatu, Daniel Mbura, kwa kuwa awali alimtambua baada ya Sabaya kumwita kwa jina lake wakiwa dukani kwa Mohamed Saad na polisi baada ya kufanyika kwa gwaride la utambuzi na polisi nao walimjulisha jina halisi la mkata rufani huyo.

Kuhusu maelezo aliyoandika, Bakari Msangi, kituo cha polisi na kutofautiana na ushahidi ulioutoa mahakamani kwa kuwa kulikuwapo na ushawishi wa kumshawishi kutokuendelea na kesi uliofanywa na askari wa polisi Kalebu, pia hawakumsomea maelezo baada ya kuandika maelezo hayo.

Kadhalika, kuhusu hoja ya mashahidi wa pili na nne kupewa dhamana na polisi na akiwamo, Deogratius, anayesemekana alipewa dhamana na alitakiwa kuunganishwa katika shauri hilo, alidai kwamba tukio lililoripotiwa awali lilikuwa shambulio la kudhuru na siyo unyang'anyi wa kutumia silaha na Deogratius alivunja dhamana.

# Viwavijeshi vyawaachia kilio wakulima Kilombero

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HEKARI 4,976 za mpunga na hekari 228 za mahindi zimeteketezwa kwa kuliwa na wadudu aina ya viwavijeshi katika Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro na kusababisha hasara kwa wakulima wa mazao hayo.

Kutokana na tatizo hilo, timu ya watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imetembelea katika maeneo yalioathirika ili kutoa elimu kwa wakulima namna ya kukabiliana nao pamoja na kuwadhibiti wadudu hao.

Akitoa elimu kwa wakulima walioathirika na wadudu hao, Mkurugenzi wa TARI kituo cha Katrin Ifakara, Dk. Kigonza Bilalo, alisema viwavijeshi hivyo vinadhibitika na viuatilifu na kuwataka wakulima kununua dawa kulingana na ushauri wa watalaamu wa kilimo.

Dk. Bilalo ambaye ni mtafiti wa mahindi na mpunga, alisema kulingana na ushauri wa kiutafiti kuna viuatilifu ambavyo vinaua viwavijeshi hao hivyo mkulima kabla ya kufanya maamuzi ya kununua dawa anapaswa kuwasiliana na maofisa ugani.

" Wapo wakulima wenzenu wamekimbilia kwenda kununua dawa bila kuwasiliana na wataalamu wa kilimo matokeo yake wadudu wameendelea kuwapo, sasa ni muhimu kuwasilina na sisi kama wataalamu wa kilimo ili tukielekeza viuatilifu pamoja na matumizi yake," alisema Bilalo.

Aidha, aliwataka wakulima hao kuchukua taadhari pale wanapoona panzi wanaanza kushambulia mazao ili kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza zaidi huku akiahidi kwenda kutoa elimu kwa wakulima wengine.

Mmoja wa wakulima hao, kutoka Kijiji cha Kilama, ambaye shamba lake limevamiwa na viwavijeshi, Husein Mohamed, alisema hiyo ni mara ya kwanza tangu ameanza kilimo hicho kwenye miaka ya 70 na anashangazwa na wadudu hao jinsi wanavyoshambulia mpunga kwa kasi ya ajabu.

Akizungumzia uharibifu huo, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi, alisema umetokea kata kata 12 za Halmashauri ya Mji wa Ifakara, lakini kata saba ndizo zimeathiriwa zaidi zikiwamo, Lumemo, Msolwa Station, Kiberege, Mang'ula, Mbasa, Kibaoni na Ifakara.

Alisema katika jitihada za awali za serikali imepeleka lita 90 za viuatilifu kwa ajili ya kuwagawia wakulima wasio kuwa na uwezo ili kudhibiti viwavi jesho hivyo huku ikiwasiliana na Wizara ya Kilimo kupata kibali cha kuagiza lita 1,500 za viuatilifu kupeleka katika maeneo mengine yaliyokumbwa na tatizo hilo.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Hoffu Mwakaje, alisema yeye na timu yake ya maofisa ugani wanaendelelea kutembelea mashamba ya wananchi waliopata athari hizo ili kutoa elimu ya njia sahihi ya kukabiliana na viwavi jeshi hivyo pamoja na kubaini maeneo mengine.


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA

COMMERCIAL DIVISION

AT DAR ES SALAAM.

TAXATION CAUSE NO. 16 OF 2018

JIELONG HOLDINGS TANZANIA LTD.........DECREE/HOLDER/APPLICANT

VERSUS

CHESSANO COTTON

GINNERY 2006 LTD.................................JUDGEMENT DEBTOR/RESPONDENT

SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION

TO:
CHESSANO COTTON GINNERY 2006 LTD,
P.O.BOX 219,
SIMIYU.

TAKE NOTICE that the Decree Holder has instituted an Application for Bill of costs against you. Service of the Summons on you has been ordered by means of this publication.
You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorized on 24th day of February, 2022 at 10:00 am when the same will be called for hearing.

TAKE FURTHER NOTICE that should you default to enter appearance in Court on the day and time mentioned above, the suit will proceed and decision may be given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 16th day of February, 2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA * COMMERCIAL DIVISION *

DEPUTY REGISTRAR

216715202



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kulia) na Mkurugenzi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania, Mara Warwick, wakibadilishana hati, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mikataba miwili ya mkopo wenye masharti nafuu. **PICHA: WFM**

# WB yaipa Tanzania mkopo nafuu tril. 1.5/-

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB) wa Dola za Marekani milioni 650 (Sh.trilioni 1.501) kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya kuboresha elimu ya msingi, pamoja na mradi wa kuimarisha usalama wa milki za ardhi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuingia kwa mikataba hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema kati ya fedha hizo dola za Marekani milioni 500 zitaelekezwa katika kuboresha elimu ya msingi na Dola za Marekani milioni 150 (Sh. bilioni 346.5) zitatumika katika kuimarisha usalama wa milki za ardhi.

Tutuba alisema miradi hiyo miwili inatekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ni sehemu ya ajenda kuu ya serikali.

Alisema: "Fedha hizi zitakwenda kuboresha na kusimamia mazingira shirikishi ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya awali na msingi; kuboresha uwezo wa walimu katika ngazi ya awali na msingi; kukuza na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na kujifunza katika shule za awali na msingi."

Aliongeza: "Pia itawezesha kukuza na kuwezesha upangaji, upimaji na utoaji hatimiliki za ardhi kwa ajili ya uwekezaji na usalama wa makazi ya watu; kuboresha na kuongeza mfumo unganishi wa taarifa za usimamizi wa ardhi; na kukuza matumizi ya TEHAMA katika upimaji na uandaaji wa hati miliki ya ardhi."

Alisema utekelezaji wa mradi wa elimu utaleta maboresho makubwa katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba 12,000 vya madarasa pamoja na vifaa vinavyohitajika vya elimu.

Alisema pia utasaidia usimikaji wa mifumo na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA katika shule na vyuo vya ualimu 800 kwa pamoja na kuongeza uandikishaji wa wanafunzi kwa shule za awali na msingi.

Kuhusu mradi wa maboresho ya usalama wa milki za ardhi, Tutuba alisema una lengo la kuimarisha mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa ardhi na kuongeza usalama wa umiliki kwa wananchi katika maeneo ya mradi.

"Mradi huu unatarajia kunufaisha nchi kupitia ongezeko la usalama wa umiliki katika wilaya 40 zilizochaguliwa, kwa kutoa hati za kimila ya kumiliki ardhi vijijini, hati za kumiliki ardhi mijini na leseni za makazi," alisema Tutuba.

Aliongeza kuwa mradi huo pia utaongeza ufanisi wa usimamizi wa taarifa za ardhi kupitia uboreshaji wa mfumo wa kidijitali wa taarifa za ardhi na utengenezaji wa ramani za msingi.

Mkurugenzi Mkazi wa WB, Mara Warwick, alisema uandikishaji wa wanafunzi shule za msingi Tanzania unaongezeka kwa kasi na kufikia milioni 2.5 mwaka 2013, kwamba kwa sasa zaidi ya wanafunzi milioni 12.3 wameingia shule ya msingi.

Alisema fedha zilizotolewa na WB zitakwenda kusaidia kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi wa shule za msingi hususani ujenzi wa vyumba vya madarasa.

## Mwalimu atakayeondoa 'zero' kulamba Sh. milioni 5 Mtwara

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amesema mkoa huo umepanga kutoa zawadi ya Sh. milioni 5 kwa shule itakayofanikiwa kufuta alama sifuri katika mitihani ya kidato cha nne kuanzia matokeo ya 2022/23

Amesema mbali na shule kuzawadiwa kiasi hicho cha fedha pia mwalimu, atakayefanikiwa kuondoa sifuri katika somo lake atakuwa ni mnufaika wa sehemu ya fedha hizo.

Gaguti, alitoa kauli hiyo jana wakati akipokea kiasi cha Sh. milioni 100 kutoka katika vyama vikuu vya Ushirika vya MAMCU na TANECU, ikiwa ni sehemu ya vyama hivyo kuunga mkono jitihada za kuinua elimu katika mkoa wa Mtwara.

Alisema matokeo ya elimu ya sekondari kwa mwaka 2022 katika mkoa wa Mtwara hayakuwa ya kuridhisha kwa kuwa asilimia 12 ya waliofanya mtihani wa kidato cha nne walipata daraja sifuri huku asilimia 60, wakipata daraja la nne.

"Pesa hizo hazitatumika katika ngazi ya mkoa wala kulipana posho bali kuhamasisha walimu kufundisha kwa bidii na kuleta matokeo bora mkoani," alisema.

Aliongeza kuwa fedha hizo alizopokea zimetokana na ushuru wa zao la korosho katika msimu uliomalizika wa 2021/2022.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja Mkuu wa TANECU, Mohamed Nassor, alisema chama chake kimetoa Sh. milioni 50 ambayo ni sawa na asilimia 3 hadi 5 ya mauzo ya korosho kwa msimu wa 2021/2022.

Alisema katika msimu huo, chama hicho kilipata Sh. bilioni 122 zilizoenda kwa wakulima moja kwa moja.

"Katika msimu huu TANECU ilivuna tani 56,000 kulinganisha na tani 50,000 zilizozalishwa katika msimu uliopita wa 2020/2021," alisema Nasoro.

Meneja Mkuu wa MAMCU, Biadia Matipa, alisema ili kutimiza malengo ya serikali ya mkoa ya kuleta mapinduzi katika sekta ya elimu wameona ipo haja ya kuchangia kiasi hicho cha pesa.

Alisema katika msimu wa 2021/2022 chama hicho kimeingiza kiasi cha Sh. bilioni 147.7 kutokana na mauzo ya korosho.

# Wanahabari waliokufa ajalini walipwa fidia

**Na Richard Makore,** MWANZA

FAMILIA za wanahabari watatu waliopoteza maisha jijini Mwanza zimelipwa fidia ya Sh. milioni 15 kama kifuta machozi.

Fidia hiyo ilitolewa jana jijini Mwanza na Benki ya Biashara Tanzania (TCB), kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Alliance Life na kukabidhiwa kwa familia hizo.

Wanahabari hao katika uhai wao walikuwa wanachama wa kikundi cha bima ya majanga ambayo inatolewa na TCB.

Katika bima hiyo mwanachama akipoteza maisha analipwa Sh. milioni 5 na familia hizo tatu za marehemu, Husna Milanzi, Anthony Chuwa na Johari Shani jana zilipokea jumla ya Sh. milioni 15.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi hundi hiyo ya Sh. milioni 15, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliishukuru benki hiyo pamoja na Shirika la Bima la Alliance Life kwa kutoa fidia hiyo.

Alisema wanahabari hao walipoteza maisha wakiwa kazini na kwamba umoja walojiunga nao umekuwa nguzo muhimu kwa sababu familia zimepata fidia.

"Fedha hizi hazilingani na thamani ya mtu yeyote, lakini kifo hakikwepeki na hili lililotokea limeacha funzo kwa waandishi wa habari," alisema Makilagi.

Aidha, Makilagi alishauri benki hiyo kuanzisha kifurushi cha faraja ambacho kitakuwa kinatoa mikopo kwa ajili ya mambo ya furaha ikiwamo harusi pamoja na kulipia ada za watoto.

Kwa upande wake, mwenyekiti wa umoja huo wa wanahabari waliojiunga na bima, Peter Saramba, aliishukuru beki hiyo pamoja na Shirika la Alliance Life kwa kutoa mkono wa pole kwa familia za wanahabari hao.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika jijini Mwanza jana, Saramba alisema walikuwa wanachama 31 na baada ya wanahabari watatu kupoteza maisha wamebaki 28.

Aliwaomba wanahabari kujiunga na umoja huo ili wanapopata majanga ikiwamo kifo, familia zao ziweze kupewa mkono wa pole.

Wanufaika wengine katika bima hiyo kinapotokea kifo ama ulemavu wa kudumu pamoja na kufiwa na mke ama mume, mama pamoja na wakwe wa pande mbili.

Akizungumza katika hafla hiyo, mwakilishi wa TCB, Francis Kaaya, alisema wanatoa mkono wa pole kwa mwanachama wa kikundi, mke, mume, mtoto pamoja na wake wanapofariki dunia.

Aliwaomba wanahabari wengine nchini ambao hawajajiunga na bima hiyo kuchangamkia fursa hiyo na kwamba fidia inatolewa kwa wakati.

Kuhusu ombi la Makilagi la kutaka ianzishwe bima ya faraja itakayokuwa inatoa mikopo kwa mtu akiwa anataka, sherehe ama jambo lolote la furaha, alisema watalifanyia kazi.

## HABARI KITAIFA

# Tulia awataka wabunge kumpa ushirikiano Rais

**Na Jenifer Gilla**

SPIKA wa Bunge , Dk. Tulia Ackson, amewaambia wabunge kuwa wanalo jukumu kubwa la kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza vipaumbele vyake alivyoviahidi kwa wananchi.

Tulia aliyasema hayo jana wakati akifungua semina ya mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati ya Uongozi, makamu wenyeviti wa kamati na Tume ya Utumishi wa Bunge ambayo inafanyika katika Ofisi ndogo za Bunge zilizopo Tunguu Zanzibar.

"Ninyi nyote ni mashahidi kwamba serikali yetu ya sasa inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ilishasema vipaumbele vyake wakati alipokuja Bungeni, basi sisi kama wabunge ni kazi yetu kuhakikisha mambo yanayoletwa kwenye kamati zetu yanazingatia vipaumbele vyake." alisema Spika.

Alisema kuwa lengo la semina hiyo ni kuhakikisha kuwa serikali inazingatia yale ambayo Rais aliyasema kwamba ndio vipaumbele vyake.

"Mtakumbuka siku mliponipa heshima ya kuwa Spika nilisema kwamba, Bunge letu ni daraja kati ya wananchi na serikali na naamini mafunzo haya yatatujengea uwezo wa kufanya kazi vizuri kama Bunge ikiwa ni pamoja na kuwafanya wale tunao waongoza sisi kama daraja baina yao na Serikali," alisisitiza.

Vilevile Spika aliwataka washiriki wote kuhakikisha wanatumia nafasi hiyo ya mafunzo vizuri ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano bora baina yao na watumishi wengine wa taasisi mbalimbali ikiwemo Bunge na Serikali.

"Tunaamini kila mmoja wenu baada ya kumaliza mafunzo haya ataweza kusimamia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu za Bunge na mtakuwa kioo kuzingatia miiko ya uongozi na utawala bora, watu watajifunza mengi kutoka kwenu," alifafanua Tulia.

Kwa upande wake, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ,Mhe. Zuber Ali Maulid, alimweleza Spika huyo kuwa Baraza lake litahakikisha linashirikiana vyema na Bunge lake katika nyanja mbalimbali za kiutendaji ili kufanikisha adhma ya Serikali ya Tanzania.

# Wavunja makaburi, waiba nondo Mwanza

**Na Richard Makore,**
MWANZA

WATU wasiojulikana wamevamia makaburi ya serikali wilayani Magu mkoani Mwanza na kuyavunja kwa lengo la kuchukua nondo zilizojengewa na kwenda kuziuza.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, amekiri kutokea tukio hilo baada ya kutembelea eneo hilo akiwa ameambatana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kwamba waliofanya tukio hilo la kinyama ni vijana wanaotafuta nondo na misalaba kwa lengo la kwenda kuziuza.

Akizungumza na Nipashe jana, Kali alisema msako wa kuwasaka watu hao umeanza na kwamba ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi hiyo usiku na mchana ili kubaini wahusika.

Mkuu huyo wa wilaya alisema alipokea taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu kuwapo uvunjaji wa makaburi hayo na kwamba alifika huko haraka na kukuta makaburi yaliyovunjwa yakiwa wazi.

Alisema watu hao wanavunja misalaba iliyotengenezwa kwa nondo pamoja na kubomoa zege la juu na kuchomoa nondo zote.

"Hawa inaonekana ni vijana wanaosaka nondo za kwenda kuuza kwa kuwa tumekuta makaburi yakiwa wazi majeneza yanaonekana na hawakuvunja jeneza hata moja," alisema.

Kali akiwa katika ziara ya kuhamisha matumizi ya anwani ya makazi katika eneo hilo, alisema, ni lazima watu hao wakamatwe ili iwe fundisho kwa wengine.

Kutokana na hali hiyo eneo hilo limeimarishwa ulinzi wa mgambo ambao wameagizwa kulinda makaburi hayo wakati ndugu wa marehemu waliozikwa hapo wakifanya utaratibu wa kuyajenga upya.



Mwanzilishi wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora, Mama Mariam Mwinyi (wapili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Maendeleo Biashara Tawi la Benki ya NBC Zanzibar, Obedy Ngavatula (kushoto), baada ya kutembelea huduma ya Mobile Clinic, inayotolewa na benki hiyo nchi nzima, wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo, mwishoni mwa wiki, yenye lengo la kusaidia wanawake, vijana na watoto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madeni ya NSSF na NHIF yalipwe mifuko ijiendeshe

**MWISHONI** mwa wiki Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), iliitaka serikali kuweka mkakati madhubuti wa kulipa madeni ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa kuwa yanaathiri utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, kamati hiyo ilisema hadi Juni 30, mwaka 2020 deni la NSSF lilifikia Sh. trilioni 1.174 ambalo lilipatikana kwa kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka huo.

Kwa NHIF deni lilifikia Sh. bilioni 209.70, huku kamati ikisema kuwa pamoja na kupunguza ufanisi wa mifuko husika, lakini yanaharibu taratibu za mizania ya fedha kinyume na kanuni za kimataifa za uandaaji wa hesabu.

Kwa ujumla madeni hayo yamesababisha mifuko kushindwa kutimiza majukumu yake kisheria kwa ufanisi kwa wakati.

Kamati hiyo ilipongeza serikali kwa kuanza kulipa deni la Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) la Sh. bilioni731 ambalo hadi Juni mwaka 2021 zililipwa Sh. bilioni 500 na mwaka huu, wametoa hati fungani maalum isiyo taslimu yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 1.176.

Majukumu ya NSSF ni kutunza michango ya wanachama wa sekta binafsi na isiyo rasmi kama wavuvi, wafugaji, wajasiriamali, wachimbaji na wengineo.

Kwa mujibu wa Sheria ya NSSF na marekebisho ya mwaka 2018, mwanachama aliyetimiza matakwa ya kikanuni anapata pensheni ya uzeeni, pensheni ya urithi, pensheni ya ulemavu, fao la upotevu wa ajira, bima ya afya, mafao ya uzazi, msaada wa mazishi.

Ili mafao yote yaweze kutolewa kwa wakati ni lazima mfuko uwe na fedha, inapotokea sasa fedha nyingi ziko serikalini na nyingine zimewekezwa kwenye miradi ambayo baadhi inalalamikiwa kwa kuwa haijaweza kutimiza lengo la uanzishwaji wake, wanaoumia ni wanachama.

Mathalani, kumekuwa na malalamiko ya watu kuachishwa kazi na kutolipwa fao la ukosefu wa ajira, fao la uzazi na pensheni zao kwa wakati, wengine wakisotea miaka na miaka bila sababu kuelezwa.

Kwa upande wa NHIF, kazi yake ni kuhakikisha wanachama wanapata bima ya afya na matibabu pale wanapokwenda kwenye maeneo husika.

Kwa muda mrefu kumekuwa na kilio cha Bima ya Afya kwa wote, imekuwa ni ombi la wabunge kwa serikali ipeleke Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na imesema iko katika hatua nzuri na utakapokamilika utapelekwa kwenye muhimili huo.


Ni muhimu serikali ikalipa madeni hayo kwa wakati, ili kurahisisha upatikanaji wa mafao kwa wanachama wa mifuko, bila kufanya hivyo ni kukwaza utendaji wa na wanaoumia ni wanachama wenyewe.

Kama ambavyo madeni ya PSSSF yameanza kulipwa basi utaratibu huo ufanyike kwa mifuko mingine, ili kusiwe na kusuasua kwa madai ya wanachama ambao kimsingi wanapaswa kunufaika na mifuko hiyo.

Kwa kufanya hivyo kutawafanya wanachama wa mifuko hiyo kuwa na imani nayo kwamba michango yao iko salama na kuwa na uhakika kupata mafao yao na pensheni kwa wakati mwafaka bila usumbufu wowote katika ufuatiliaji.

Ni matarajio yetu kwamba serikali itachukua hata haraka kuhakikisha madeni hayo yanalipwa ili mifuko hiyo ijiendeshe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuwachapa viboko wanafunzi sawa wakati mwingine, lakini...

Na Sabato Kasika

**SUALA** la kuwapo ama kuondolewa adhabu ya viboko shuleni ni mjadala miongoni mwa wadau, unaowagawa watu katika makundi ya wanaunga mkono na wanaopinga adhabu hiyo.

Viboko vimekuwa ni mjadala kutokana na matukio ya kufariki dunia au kuumizwa baadhi ya wanafunzi na hivyo kuwafanya wadau wa elimu kutoona umuhimu wake na wengine kuamini kwamba bado adhabu hiyo inafaa.

Katika msimamo wake, Rais John Magufuli, enzi ya uhai wake, aliwahi kusema, viboko vinafundisha na kuwa ipo haja ya kuifanyia marekebisho sheria inayozuia adhabu hiyo.

Ni katika ziara yake mkoani Mbeya wakati huo, anasema: "Nafikiri kama kuna mahali tulikosea ni ile sheria, inabidi ikafanyiwe marekebisho wawe wanatandikwa viboko".

Hatua hiyo ilitokana na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuwachapa viboko 14 na kuwarudisha nyumbani wanafunzi 392 wa Sekondari ya Kiwanja Chunya kwa madai ya kuchoma moto mabweni ya shule hiyo.

Mbali ya kupewa adhabu hiyo, wanafunzi hao walitakiwa kulipa Sh. 200,000 kila mmoja kwa ajili ya kukarabati mabweni mawili ambayo walituhumiwa kuyateketeza kwa moto.

Binafsi naunga na kauli hiyo, kwa kuwa adhabu ya viboko kwa mwanafunzi, si mbaya kama itatolewa kwa lengo la kumrekebisha, lakini ikiwa ni ya kumkomoa, matokeo yake ni kuumia na kuchochea mjadala zaidi.

Kwenye Biblia kitabu cha Mithali 23: 13 kinashauri: "Usimnyime mtoto wako mapigo; maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa".

Hivyo suala la kuwapo adhabu ya viboko kwa wanafunzi ni jambo la kawaida, ikitolewa kwa utaratibu unaotakiwa, inaweza kupunguza matukio ya uharibifu wa mali za shule mambo mengine yasiyotakiwa.

Vilevile, adhabu hiyo ikitolewa kwa utaratibu unaotakiwa, itapunguza pia matukio athari ya viboko kwa wanafunzi shuleni kama vile kuumizwa kwa baadhi yao na hata kuachwa na makovu.

Ni jukumu la mzazi na mlezi kumpa fursa ya kusoma mtoto wake na pia mwalimu anatakiwa kutimiza wajibu wake kwa uadilifu wa kumpa elimu, kumtunza, kumlea na kumuongoza kwa kumkuza na kumwendeleza.

Si dhamira ya mwalimu kumdhuru mwanafunzi kwa viboko, bali kumjenga na kumrekebisha, kwa kuwa mwalimu ni mlezi wake shuleni, hivyo hata adhabu anayotoa inatakiwa kumrekebisha na siyo kumkomoa.

Akiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako, alishaonyesha kukerwa na baadhi ya walimu wanaoshindwa kufuata mwongozo wa adhabu ya viboko shuleni.

Mwongozo huo upo katika waraka namba 24 wa mwaka 2002, unaoweka wazi kuwa adhabu ya viboko inaweza kutolewa endapo kutatokea utovu wa nidhamu uliokithiri ama kwa makosa ya jinai yaliyotendeka ndani au nje ya shule na yenye mwelekeo wa kuishushia shule heshima.

Anaweka wazi kuwa waraka huo pia unaongeza kwamba viboko vitatolewa kwa masharti ya kuzingatia ukubwa wa kosa, umri, jinsi na afya ya mtoto na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja.

Pamoja na hayo anabainisha kuwa waraka unamtambua mwalimu mkuu kama mwenye mamlaka ya kutoa adhabu ya viboko na unamtaka pia atie saini katika kitabu maalum kila adhabu ya viboko inapotolewa.

Aidha, anasema, waraka huo unaweka wazi kuwa, mwanafunzi ama mzazi anapokataa adhabu ya viboko, sharti asimamishwe shule ili kupisha hatua nyingine za kinidhamu juu ya kosa lake.

Walimu pia wanaonywa kuwa hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao kama watakiuka utaratibu ulioidhinishwa na waraka huo, na ni marufuku kuonekana wakiwa na fimbo mkononi kwa lengo la kumwadhibu mwanafunzi.

Muungwana anaamini kwamba, kutozingatia mwongozo huo, ndiyo chanzo cha kuwagawa watu na kuzusha mjadala katika jamii wa kutaka adhabu ya viboko iendelee ama ifutwe.

Wakati huu ambao serikali inalifanyia kazi pendekezo ka kupitia kanuni na miongozo ya uchapaji viboko, si vibaya ikaweka washauri nasaha shuleni watakaokuwa wakisikiliza malalamiko ya wanafunzi.

HABARI KITAIFA

# Wamiliki wa vyombo vya usafiri majini wasisitizwa utaratibu

Na Maulid Mmbaga

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limewataka wamiliki wa vyombo vya usafiri majini kuzingatia kanuni, miongozo na sheria za uendeshaji wa vyombo hivyo ili kuhakikisha usalama wa Watanzania, na kwamba litawawajibisha wamiliki watakaoenda kinyume.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam Mkurugenzi Mkuu wa (TASAC), Kaimu Mkeyenge, alisema chombo chochote kinachomilikiwa na serikali au binafsi ni lazima kiwe salama akidai kuwa kama hakitakuwa salama maisha ya wananchi yatakuwa hatarini.

Pia alitoa msimamo kwamba watahakikisha wanasimamia kanuni kwa kuiwakilisha nchi kwasababu ni mwanachama wa Shirika la Bahari Duniani (IMO).

"Huwa tunakaguliwa kila baada ya miaka fulani sasa wakikuta kwamba hatudhibiti hilo eneo taarifa zake hazitachukuliwa kama za TASAC au wizara itakuwa ni nchi hivyo tunaharibu uwakilishi wetu kule na tunaingia kwenye orodha ya nchi ambazo hadhikidhi vigezo vya kuwa mmoja wa wanachama kwasababu tunaendesha sekta kiholela.

"Hiyo ni hatari kwa uchumi wa nchi kwa sababu ulinzi na usalama wa vyombo unajumuisha mambo mengi na wanaweza wakakaa wakaongea kwamba eneo au ukanda fulani hauko salama kwa sababu wao wenyewe kijidhibiti hawawezi, kwa hiyo vile vigezo tukivizingatia itasaidia kuinua nchi katika maeneo hayo," alisema Mkayenge.

Pia alisema kunapokuwa na vyombo ambavyo ni salama na kujihakikishia kuwa vimekidhi vigezo wanawaweka wananchi katika hali bora na salama, kuokoa maisha pamoja na mali zao, akidai kwamba kutokana na kaguzi mbalimbali walizozifanya walisimamisha kivuko cha MV Kazi baada ya kubaini kuwa hakipo salama.

Aliongeza kuwa sheria iliyofanyiwa marekebisho imewapa jukumu la kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo ambavyo vinatembea majini ikiwamo vivuko ambavyo vinamilikiwa na kuendeshwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).

"Tumeona sasa ni muda mwafaka kutoa uelewa kwa watumiaji wa vyombo, lakini wamiliki kwamba sasa (TASAC) inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ambayo inaonyesha mapungufu na yanatakiwa yafanyiwe kazi kisheria, kinyume na hapo tutatoa adhabu ikiwamo kusimamisha kivuko.

"Katika sekta yetu ya uchukuzi hususani usafiri kwa njia ya maji tunasema kilichoko kwenye ardhi kina usalama zaidi kuliko kuingia kwenye maji, unapokuwa kwenye maji hauko salama hata kama uko kwenye chombo salama," alitahadharisha Mkeyenge.

## Leseni 2,000 za uchimbaji mdogo hazijaendelezwa

Na Jumbe Ismailly, IRAMBA

MKOA wa Singida una jumla ya leseni 2,089 za uchimbaji mdogo wa madini zisizofanyakazi, jambo linalosababisha maeneo mengi kushikiliwa bila shughuli za uchimbaji kufanyika.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Singida, Chone Malembo, aliyasema hayo kwenye taarifa aliyotoa kwa Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, wakati wa kongamano la siku moja kujadili fursa na changamoto kwenye sekta hiyo lililofanyika katika mji mdogo wa Kiomboi, wilayani Iramba.

"Wilaya ya Iramba inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya leseni za uchimbaji mdogo katika Mkoa wa Singida, leseni zinazofanyakazi ni chache sana na hivyo kufanya maeneo mengi kuwa yameshikiliwa bila kuchimbwa," alisisitiza Chone.

Akifafanua, Meneja huyo alisema Wilaya ya Iramba ina jumla ya leseni 694 kati yake 102 zinafanya kazi na 692 hazifanyi kazi, huku Wilaya ya Manyoni ziko 539 zinazofanyakazi ni 75 na 463 hazifanyikazi.

Aidha, Chone alisema Ikungi kuna leseni 581 zilizoko kati yake 108 zinafanyakazi na 473 hazifanyikazi, Wilaya ya Mkalama ni 495 zinazofanyakazi ni tano huku 490 hazifanyikazi, Wilaya ya Singida zipo 139 zinazofanyakazi ni 68 na 71 hazifanyikazi.

Kwa mujibu wa Chone, wachimbaji katika Wilaya ya Iramba hususani wadogo wanapata hadha kubwa na kushindwa kuzalisha kutokana na uwepo wa maji mengi chini ya ardhi.

Akifungua kongamano hilo la siku moja, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alisema tangu enzi za ukoloni Wilaya ya Iramba, ilijulikana kuwa na utajiri wa madini na kwa historia mgodi wa kwanza wa dhahabu Tanzania ulianzishwa miaka ya 1909 katika eneo la Sekenke, wilayani Iramba.

Kwa mujibu wa Dk. Kiruswa, takwimu zinaonyesha kwamba kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi 2022 jumla ya gramu 1,037,000 sawa na tani 1.1 zenye thamani ya Sh. bilioni 7.69 ikiwa ni mrahaba na ada ya ukaguzi zilikusanywa.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imeweza kukusanya jumla ya Sh. milioni 328.4, ikiwa ni ushuru wa huduma kutokana na uzalishaji huo.





**Tangu kampuni ya Barrick** ilipoingia ubia na Serikali ya Tanzania, mwaka 2019, ilijikita katika kufufua na kukuza uzalishaji katika migodi ya North Mara, Bulyanhulu na Buzwagi. Kwa hakika, jitihada hizo zilizaa matunda. Kwani, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2020, kampuni ya Barrick iliweza kuilipa Serikali gawio la Dola milioni 250 pamoja na awamu ya kwanza ya Dola Milioni 300 kama malipo yaliyotokana na maafikiano (settlement) na Serikali. Aidha, kampuni ya Barrick imewekeza zaidi ya Dola za kimarekani bilioni 1.8 katika uchumi wa nchi na kutumia kiasi cha Dola za kimarekani milioni 6.7 katika masuala mbalimbali ya kijamii. Kwa upande wa raslimali watu, Barrick, imetengeneza ajira mpya 600. Hatua hii imefanya asilimia 96 ya wafanyakazi wote migodini kuwa ni Watanzania.

Upande wa uzalishaji, kuna uwekezaji mkubwa unaofanywa katika migodi ya North Mara na Bulyanhulu ili kuiwezesha migodi hiyo, kufikia hatua ya daraja la hali ya juu kabisa ya uzalishaji wa dhahabu (**Tier 1 Gold Complex*). Hatua hii, itaifanya migodi ya Barrick yenye hadhi hiyo duniani kuwa saba.

BARRICK
Tunajenga Mustakabali
www.barrick.com | NYSE : GOLD • TSX : ABX

* *Mgodi wa daraja la juu (Tier One Gold Asset), ni mgodi wenye uwezo wa kuzalisha wakia 500,000 za dhahabu kwa mwaka kwa gharama iliyo chini ya wastani wa gharama za uzalishaji katika sekta ya madini ya dhahabu kwa kipindi cha wa uhai wa mgodi huo ambao ni angalau miaka kumi.*

216716101

# Sababu ushirika kusuasua ukusanyaji wa korosho

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Msingi cha Ushirika Umoja cha mjini Liwale mkoani Lindi, kimeshindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa korosho kilichojiwekea msimu wa 2021/2022 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uzalishaji duni.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Myao, alisema hayo alipozungumza na gazeti hili, kuwa katika msimu huo uliomalizika hivi karibuni, walitarajia kukusanya tani 3,000 za korosho, lakini wamejikuta wakishia tani 1,758.

"Hii imetokana na mvua kutonyesha kwa wakati na kusababisha uzalishaji kuwa duni, lakini ninaamini wakulima wetu hawatakata tamaa, badala yake hali hiyo itakuwa ni fursa kwao kujipanga kwa ajili ya msimu ujao," alisema Myao.

Alisema, kupanda au kushuka katika ukusanyaji wa korosho ni jambo la kawaida ambalo halipaswi kuwakatisha tamaa wakulima wa chama hicho na kwamba, viongozi wataendelea kuwahimiza kuongeza uzalishaji.

"Unajua penye wengi pana mengi, inawezekana wakawapo wa kukata tamaa kutokana na hali ya hewa ilivyokuwa msimu uliopita, lakini sisi viongozi wao hatuna budi kuwatia moyo wakulima wetu," alisema.

Alifafanua kuwa uzalishaji duni wa korosho, ni miongoni mwa ajenda ambazo zinatarajiwa kufikishwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho utakaofanyika mwishoni mwa mwezi ujao.

Aidha, Mwenyekiti huyo alisema, katika msimu huo uliopita, kilo moja ya korosho daraja la kwanza ilikuwa inauzwa kuanzia shilingi 1,600 hadi shilingi 2,395, huku daraja la pili ikiuzwa shilingi 1,300.

"Pamoja na kasoro hizo za uzalishaji na bei ndogo ya korosho, chama chetu kinaendelea kuimarika kwani kina jumla ya wanachama 1,042 na maghala makubwa mawili ya kuhifadhia mazao ya wakulima," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema, hakuna chama cha msingi cha ushirika kinachoweza kufikia mafanikio ya umoja, kwa madai kwamba chama chao kina vitega uchumi vingi ikiwamo mashine ya kukamua mafuta ya alizeti.

"Vilevile, maghala yetu nayo ni miongoni mwa vitega uchumi vikubwa, kwani wakulima ambao si wanachama wa Umoja, wanaotunza mazao yao katika maghala hayo, wanalipia, lakini tuna majengo ya kupangisha," alisema.

Myao alisema: "Kwa ujumla ni kwamba, chama chetu cha Umoja kina mali mbalimbali zikiwamo zisizohamishika na zinazohamishika, zenye thamani ambayo inaweza kuzidi Sh. bilioni moja."



Waziri wa Nishati na Madini wa Sudan Kusini, Martin Gama Abucha (wapili kushoto), akipata maelezo ya shughuli za kampuni ya madini ya Barrick kutoka kwa Meneja Uhusiano, Neema Ndossi (katikati), wakati alipotembelea maonyesho ya kimataifa ya uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania 2022, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa wa Barrick, Abela Mutiganzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mil. 100/- kujenga wodi ya mama na mtoto Dar

**Na Salome Mwasamale**

SERIKALI imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Mbezi Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam ili kuondoa kero mbalimbali wanazokutana nazo wajawazito wakati wa kujifungua.

Pia imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala, wodi ya mama na mtoto na maabara katika zahanati ya Mpigi Magohe ambayo imepandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Diwani wa Kata ya Mbezi, Ismail Malata, alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye mkutano wake wa kwanza katika mwaka huu.

Malata alisema yupo kwenye mchakato wa kuhakikisha Mtaa wa Msumi nao unapata zahanati hivyo aliwaomba wananchi kujitolea eneo ili kufanikisha zoezi hilo.

"Najua wananchi mnayo maeneo hivyo naomba muisaidie serikali kwa kujitolea maeneo ili na wao wawajengee zahanati kwa kuwa fedha zipo fanyeni hivyo kwa manufaa yetu na watoto wetu," alisema.

Akizungumzia kuhusu elimu, alisema wapo kwenye mapambano ya kuinua kiwango cha ufaulu na kuteketeza ziro katika kata hiyo zoezi ambalo linafanyika kupitia mikakati mbalimbali ikiwamo ya kuongeza idadi ya shule, madawati na kuboresha nidhamu.

Aidha, aliipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kuwapatia shilingi milioni 400 fedha za mfuko wa ujenzi wa madarasa ya UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Makabe Sekondari ambayo imekamilika na tayari imeanza kutoa huduma hivyo kufanikisha kata ya Mbezi sasa kuwa na sekondari tatu.

"Naomba nimshukuru sana mama Samia Suluhu Hassan kwa kutukumbuka na sisi na kutupatia fedha hizi ambazo zimefanikisha Kata ya Mbezi sasa kuwa na shule tatu za sekondari na kupunguza changamoto ya umbali kwa watoto wetu," alisema.

Pia alisema shilingi 470 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Msakuzi fedha ambayo itafanikisha upatikanaji wa madarasa, madawati, jengo la utawala, matundu ya vyoo na maabara tatu.

## Utumishi wakumbushwa kumsaidia Samia usimamizi wa rasilimali watu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema watumishi wa ofisi yake wanao wajibu wa kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kujenga na kusimamia vema rasilimali watu katika sekta zote ili itumike kuleta maendeleo endelevu.

Jenista alisema hayo jijini Dodoma katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2022), iliyoandaliwa na menejimenti ya ofisi yake kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya utendaji kazi kwa watumishi wa ofisi yake.

Waziri Jenista amesema, juhudi zinazofanywa na Rais kujenga rasilimali watu katika sekta za elimu, afya, kilimo, madini, maji, nishati, anga na miundombinu ya barabara na reli zinapaswa kuungwa mkono kwa vitendo na watumishi wote wa umma nchini ili kuchangia ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo endelevu.

"Wajibu wetu sisi ni kumsaidia Rais Samia kuimarisha rasilimali watu serikalini ili sekta zote zitoe mchango chanya katika ujenzi wa uchumi imara na maendeleo ya taifa kwa ujumla," alisisitiza Mhagama.

Alitoa wito kwa watumishi wa ofisi yake, kujenga umoja na mshikamano ili kuweka mazingira rahisi na rafiki ya utendaji kazi ambao utakuwa unaunga mkono kwa vitendo jitihada za Rais Samia kutoa huduma bora kwa wananchi na kuleta maendeleo kwa taifa.

"Tupendane na tuishi kama ndugu kwani mafanikio ya kila mmoja wetu ni mafanikio ya ofisi yetu na utumishi wa umma kwa ujumla, tuna kila sababu ya kufanya kazi kwa bidii, weledi, uzalendo na kwa kuzingatia miiko, Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi ikiwa ni pamoja Sheria, Taratibu na Miongozo ya utumishi wa umma iliyopo kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa letu," alifafanua.

Aidha, amewataka watumishi wa ofisi yake kuwa kioo na mfano bora wa kuigwa kiutendaji na watumishi wa taasisi zote za umma nchini, kwani ofisi yake ndio imepewa jukumu kubwa la kumsaidia Rais kusimamia masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI ndio wamebeba dhamana ya maisha ya watumishi wote wa umma na ustawi wao hivyo amewataka kuendelea kuchapa kazi kwa bidii.

Naye Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, aliwashukuru watumishi wa ofisi yake kwa kufanya kazi kwa bidii katika mwaka uliopita wa 2021 na kuwakumbusha kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kutoa huduma bora.

## Mkutano kupokea mrejesho mradi ukatili kingono

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Kinondoni Dar es Salaam, Abbas Tarimba, anatarajiwa kufungua mkutano wa kutoa mrejesho wa awali kuhusu utekelezaji wa mradi wa majaribio ya kukabiliana na ukatili wa kingono unaofanyika Kinondoni.

Mkutano huo ambao utafanyika leo, Makumbusho Dar es Salaam unatarajisha kushirikisha wadau mbalimbali baadhi yao ni watendaji wa kata, wenyeviti wa serikali za mitaa, madaktari, wauguzi, maofisa elimu, walimu na wanasheria.

Akizungumza na gazeti hili, mratibu wa mradi huo Dk. Geofrey Chambua, alisema unatekelezwa na Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC), kwa kushirikiana na Shirika la Maendele la Japan (JICA), katika kata za Makumbusho na Mwanyamala wilayani Kinondoni.

"Tumemualika mbunge wa Kinondoni kutufungulia mkutano wetu ambao wadau watarejesha tathmini ya kile walichokifanya na walichokiona tangu mradi uanze mwishoni mwa mwaka jana," alisema Dk. Chambua.

Akifafanua zaidi, alisema ulianza kwa kufanya upembuzi awali ili kubaini hali halisi ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na muitikio wa taasisi za uwajibikaji na utoaji wa huduma katika eneo la mradi.

"Vilevile kuwa na kuutambulisha mradi kwa wadau wote wa mradi na Kufanya vikao vya mara kwa mara kuelezea maendeleo ya mradi katika awamu zote za mradi," alisema.

Aliongeza kuwa waliwajengea uwezo watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala wakiwamo madaktari, wauguzi, wataalamu wa maabara na watumishi wa kada nyingine zinazoendana na mradi.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa kutambulisha mradi huo kwa wajumbe wa Kamati ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Wakili Anna Henga, alisema wamewajengea uwezo askari polisi zaidi ya 50.

Polisi hao ni wale wa Dawati la Jinsia na Watoto Katika Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni ambao wamejengwa uwezo wa jinsi ya kushughulikia kesi za udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.

Wakili Henga pia alisema, mradi umetoa mafunzo kwa watendaji na wenyeviti wa serikali za kata na mitaa yote 13 ya Mwananyama la Makumbusho, na kwa waajumbe zaidi ya 50 wa Kamati ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) katika kata hizo mbili.

Aliongeza kuwa matarajio yake ni kuona mradi huu unakuwa msaada kwa manusura wa udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono na kutoa elimu kwa jamii katika kata hizo, ili kupambana na kutokomeza vitendo hivyo na kuhakikisha huduma na haki kwa walengwa zinapatikana kwa ufanisi na wakati muafaka.

# CCM yamuunga mkono Rais Samia kimataifa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kuwa kimeridhishwa na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye medali za kimataifa ambazo zimeifanya nchi kupata manufaa yakayoharakisha maendeleo ya wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kumpokea Rais Samia akitokea nchi za Ufaransa na Ubelgiji, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alisema uthubutu, sera nzuri na utendaji wenye tija ndiyo umeifanya Tanzania kuaminika kimataifa.

Alisema kazi inayofanywa na Rais Samia siyo nyepesi bali kubwa inayotakiwa kuungwa mkono kwa kuwa ameithibitishia dunia msimamo wa taifa na sera nzuri zenye ushawishi hata ndani ya Afrika.

Kwa mujibu wa Shaka, licha ya kuonyesha upeo, maarifa na ufahamu mpana, Rais Samia aliweka bayana msimamo wa nchi yake kwenye dhamira ya kudunisha NA kuendeleza ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

"Rais Samia kila alipopita akikutana na wakuu wa nchi wenzake, pia alikutana na makundi mbalimbali na kutoa hotuba za kizalendo akiweka msisitizo wa mshikamano wa kikanda na kimataifa na kumfanya ajipambanue kimataifa," alifafanua Shaka.

Aliongeza: "Rais Samia ni alama mpya ya nchi yetu na kioo cha Afrika kwenye medani za kimataifa amekuwa mchapakazi anayesimamia utekelezaji wa sera zilizomo kwenye ilani ya uchaguzi."

Aidha, Shaka alisema Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania imelenga kuendeleza diplomasia ya uchumi, baada ya kupata mfanikio makubwa ya kujitangaza kimataifa, kuelezea sera na misimamo yake tokea awamu ya kwanza hadi ya sita.

Alisema Rais Samia amejenga ukaribu na viongozi wa mataifa wenye uchumi imara duniani, baada ya kufanikiwa kukutana na marais wenzake kadhaa kutokana na msingi uliowekwa watangulizi wake.

"Kama nilivyosema Rais hatazuiwa kwenda mahali popote atafanya hivyo kwa sababu dunia ya sasa si ile ya kujifungia Ikulu anapaswa kuingia kwenye mawindo ya diplomasia ya uchumi. Ulimwengu wa leo ni kijiji kimoja kinachotegemeana na wala si muda wa kujitenga," alibainisha Shaka.

Alisema, Rais Samia amekuwa akishiriki kwenye meza na majukaa mbalimbali ya majadiliano ya kisiasa, kibiashara na ya kiuchumi kwa manufaa ya Watanzania.




Wafanyabiashara wadogo wa Kihesa, Manispaa ya Iringa, wakihamisha kibanda chao kilichokuwa kando ya barabara kuu ya Iringa -Dodoma jana, baada ya Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), mkoani humo kutaka vibanda vyote vilivyo ndani ya mita 60 kuondolewa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# RC aingilia kati udumavu kwa watoto

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameiagiza Kamati ya Afya ya Msingi katika mkoa huo (CHMT) kuweka mkakati madhubuti wa utoaji wa elimu ya lishe kwa wananchi ili kukabiliana na udumavu kwa watoto.

Kunenge alitoa agizo hilo juzi mjini Kibaha wakati wa kikao cha tano cha tathmini ya hali ya lishe katika mkoa huo kuanzia Julai hadi Desemba 2021.

Alisema licha ya kusainiwa kwa mkataba wa lishe, bado mkoa huo unakabiliwa na tatizo la utapiamlo na udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano ambapo kila watoto 100 wanaozaliwa 25 wanazaliwa na udumavu.

"Kila mmoja anatakiwa kusimamia vizuri majukumu yake kwani pamoja na kusaini mkataba wa lishe, utekelezaji wake bado ni mzito, mipango inayopangwa inategemea kutekelezwa na rasilimali watu tuwajibike katika nafasi zetu," alisema Kunenge.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, alisema mkoa huo umeanza mpango wa kutoa ellimu ya lishe kwa wakazi wake kwa kuwatumia maofisa lishe kuanzia ngazi ya mkoa hadi ngazi ya vijiji jambo ambalo wanaamini linaweza kupunguza tatizo hilo ndani muda mfupi.

Ofisa Lishe wa mkoa huo, Pamela Meena, alisema hali ya udumavu kwa mkoa ni asiimia 23.8 chini ya kiwango cha Taifa cha asilimia 30.1 (TNNS, 2018).

Pamela alieleza kuwa katika watoto 196,524 wenye umri chini ya miaka mitano watoto wa mkoa huo 46,773 wamedumaa na hawana uwezo wa kufundishika na hata kuinua uchumi wa familia na taifa kwa ujumla watakapokuwa watu wazima.

# Umeme wa jua kuinufaisha Meatu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, wanatarajiwa kuondokana na ukosefu wa huduma ya umeme, baada ya serikali kuahidi kupeleka mradi mkubwa wa umeme wa Megawatts 150.

Sophia Mjema, alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi, uliofanyika katika Kijiji cha Ipeja wilayani Kishapu.

Alisema changamoto ambayo wameisema wananchi hao juu ya ukosefu wa huduma ya umeme, serikali hivi karibuni italitatua ambapo kuna mradi mkubwa wa umeme wa jua unakuja wilayani humo, na vijiji vyote vitaunganishwa na huduma hiyo na hakutakuwa tena na malalamiko ya ukosefu wa umeme.

"Changamoto ya ukosefu ya huduma ya umeme kwenye vijiji vyote vya wilaya hii ya Kishapu itakwisha, ambapo hivi karibu Waziri wa Nishati atakuja kuzindua mradi mkubwa wa umeme wa Jua wenye Megawatts 150, na umeme huu ni kwa ajili ya wananchi wa Kishapu tu," alisema Mjema.

Asuala la ukosefu wa zahanati kwenye kijiji hicho, alisema kuwa serikali italifanyia kazi, kwa sababu ndiyo ajenga kubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma za afya karibu, na ndiyo maana sasa hivi katika maeneo mengi kuna ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Alizungumzia pia tatizo la ubovu miundombinu ya barabara hasa kutoka kwenye kibao cha Shule ya Msingi Ipeja hadi shuleni, na kuaaliagiza giza barabara hiyo ifanywe matengenezo ya haraka, ili kuondoa changamoto ya wanafunzi kupata usumbufu wa kwenda shule hasa kipindi hiki cha msimu wa mvua.

Alisema katika changamoto ya ukosefu wa huduma ya majisafi na salama, wananchi watapata maji hayo kwa sababu serikali imeshasaini miradi 10 ya maji na makandarasi, na kwamba maji hayo yawafikia pia wananchi hao.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa, aliwataka wananchi wote mkoani Shinyanga, kuwa siku ya zoezi la kuhesabiwa sensa ambalo litafanyika Agosti mwaka huu watoe ushirikiano wa kuhesabiwa, ili serikali ipate idadi kamili ya watu na kuwa virahisi kutoa huduma kwa jamii.

Awali Mwenyekiti wa Kijiji cha Ipeja, Juma Bundallah, akiwasilisha kero za wananchi wake kwenye mkutano huo wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, alisema wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya umeme, majisafi na salama, zahanati pamoja na ubovu wa miundombinu ya barabara hasa ya kwenda shuleni.




Mabasi yakiwa yameegeshwa katika Kituo cha mabasi cha Makambako, mkoani Njombe jana, ambacho mazingira yake ni mabaya kutokana na kuwa na mashimo makubwa yanayopelekea kujaa maji wakati wa mvua, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa abiria na madereva. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UVIKO-19 ulivyopunguza idadi watalii

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa kutokana na janga la UVIKO - 19 upande wa Tanzania idadi ya watalii waliotembelea nchini ilipungua kutoka 1,527,230 mwaka 2019 hadi 620,867 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 59.3 na mapato yatokanayo na utalii yalipungua.

Kwamba yalipungua kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019 hadi dola bilioni 0.715 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 72.5.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, wakati wa uzinduzi wa mafunzo kwa watoa huduma za utalii nchini kuhusu mwongozo wa kukabiliana na UVIKO katika sekta ya utalii mkoa wa Njombe.

"Tumeshuhudia kuyumba kwa biashara za utalii na hata kufungwa kwa baadhi ya kampuni za utalii na hoteli. Hata hivyo kwa sasa sekta ya utalii nchini imeanza kuimarika kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Alisema kuwa mafunzo hayo yatawajengea uwezo watoa huduma za utalii nchini juu ya namna bora ya kukabiliana na janga la UVIKO-19 kwa kuzingatia matakwa ya kiafya na usalama pamoja na kuboresha huduma zimazotolewa na hatimaye kuimarisha ushindani wa nchi katika masoko mbalimbali.

"Ni matarajio ya serikali kuwa mafunzo haya yatakapokamilika yatachangia kuboresha utoaji huduma katika mnyororo wa utalii na kusababisha nchi kuongeza idadi ya watalii na kufikia malengo ya kupata watalii milioni tano mwaka 2025," alisema Kasongwa.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, aliwataka watoa huduma kuwa wakarimu ili kujiongezeka kipato kwa kuwa ukarimu ni biashara.

Mkurugenzi wa mafunzo na shughuli za kitaalamu, Dk. Florian Mtei, kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii alisema mafunzo hayo yatawezesha kuchangia uboreshaji utoaji huduma katika sekta ya utalii hasa kipindi cha baada ya athari za Uviko-19.

"Kwa kipindi hiki cha janga la UVIKO-19, wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii upo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii wenye dhamana ya kutoa mafunzo ya ukarimu na utalii nchini, kutoa huduma za ushauri na kufanya utafiti mbalimbali katika fani ya ukarimu na utalii nchini na kubaini kuwa watoa huduma sio wakarimu," alisema Mtei.

Wizara ya Maliasili na Utalii ya kupitia chuo hicho imeandaa mafunzo hayo ya siku tano kwa wadau, wakuu wa sekta ya utalii na ukarimu na watoa huduma katika mnyororo mzima wa utalii, ambayo ni sehemu vya utekelezaji wa mradi wa UVIKO-19 awamu ya kwanza.

# Kilimo cha misitu sasa kuongezwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI inakusudia kuongeza idadi ya wakulima wanaojishughulisha na kilimo misitu nchini kutoka milioni nne kufikia milioni 15 ambao watasaidia kupunguza uharibifu wa misitu na kuongeza kasi ya uhifadhi wa mazingira.

Kauli hiyo ya serikali imetolewa na Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, wakati akifungua mkutano wa wadau kwa ajili ya kupitia rasimu mbalimbali za kuendeleza sekta ya misitu nchini unaofanyika mjini Morogoro.

Alisema kwa sasa uharibifu wa misitu kwa mwaka ni takribani hekta 462,000 kiwango ambacho ni kikubwa na kwamba lazima kuwapo na mkakati wa kuhakikisha misitu hiyo inaokolewa.

Dk. Mwakalukwa alisema moja ya mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza kilimo misitu ambacho kikiweza kuwafikia watu wengi kupunguza presha ya watu kupata mahitaji ya rasilimali za misitu au watu kwenda msituni kukata kuni na matumizi mengine.

"Tukiweza kuwafikia watu wengi wakafanya shughuli za kilimo misitu itasaidia kupunguza presha ya matumizi ya miti katika misitu yetu kwa kuwa mkulima atalima na kupata mazao yake kama kawaida na wakati huo huo atakuwa anapata mahitaji yake ya kuni au kuchoma mkaa kupitia shamba lake hilo hilo," alisema.

Aliwatoa hofu wakulima hao kuwa hakuna madhara yoyote ya kuchanganya mazao na miti bali kinachotakiwa ni kujua ni aina gani ya miti ambayo wakati wa upandaji utachanganya na hayo mazao ambayo utavuna kwa nyakati tofauti huku ukipata faida mara mbili.

Kwa upande wake Dk. Felician Kilahama, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), alisema bila kuwapo kwa misitu hakuna shughuli za kilimo, hakuna chakula na ukame utaongezeka kwa kuwa hakutakuwa na maji hivyo ni muhimu kutengeneza mazingira ya kuendelea kuitunza misitu.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI, Dk. Revocatus Mushumbuzi, alisema kuwa licha ya kuongezeka kwa mazao ya siti mbao nchini Tanzania lakini kumekuwa na changamoto katika matumizi endelevu ikiwapo kutotoa kipaumbele cha kutosha katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao hayo ili kuongeza mchango wake kiuchumi katika pato la Taifa.

Nipashe
TESA
Jumanne Februari 22, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
Kamati ulinzi mwanamke, mtoto ziingie kazini kustawisha jamii



Ukurasa 13
Mwisho enzi za ukatili; Bila cheti cha kuzaliwa hakuna ndoa



Ukurasa 14
Maafa tabianchi yanavyoiweka Afrika kwenye kona mbaya

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

UCHUNGU JUU YA UCHUNGU

# Safari ya wajawazito kubebwa na ng'ombe kwenda zahanati

ELIMU na kampeni za uzazi salama hapa zinaelekea kugonga mwamba. Ni kwa sababu licha ya serikali na wadau kufundisha elimu ya afya ya uzazi kwa wajawazito ili kuzijua dalili hatarishi wakati wa ujauzito kuna maeneo taarifa hizo hazifanyi kazi wala kuwanufaisha walengwa.

Dalili hatarishi kama upungufu wa damu, kutokwa damu ukiwa mjamzito, kuugua malaria mara kwa mara, shinikizo la juu la damu na kifafa cha mimba, lakini yote tisa kinamama wa baadhi ya maeneo hawawezi kujifungulia hospitalini.

Hawafiki kwa watalaamu wala kujifungulia hospitalini kutokana na kukosekana, zahanati na vituo vya afya, hivyo kukwamisha juhudi za elimu ya uzazi salama kupunguza vifo vya wazazi na watoto.



Wajawazito kusafirishwa na mikokoteni ya kubebea mizigo karne ya 21 ni jambo la kutafakari zaidi. **PICHA: MTANDAO**

### 'AMBULENSI' ZA NG'OMBE

Wanawake wa Kijiji cha Ng'wamadelanha wilayani Shinyanga, hasa wajawazito wana mengi ya kusimulia yanayohuzunisha, licha ya kusikia taarifa za elimu ya uzazi salama.

Baadhi wanaweza kusema wanajuta kuwa na hali hiyo kutokana na ukosefu wa huduma za afya, zinazoweka rehani maisha yao na ya watoto tumboni, lakini kubebwa kwenye mikokoteni wakiwa na uchungu wa uzazi.

Kikubwa zaidi ni kukosa hospitali na kulazimika kusafiri zaidi ya kilometa 20 kufuata huduma za matibabu zilizoko kwenye kijiji jirani. Wanatembea takribani kilometa 40 kwenda na kurudi kufikia matibabu kwenye zahanati ya Kijiji cha Shilabela, wakipita Kijiji cha Sayu ili kuifikia zahanati hiyo.

Hayo yanatokea wakati Sera ya Afya ya mwaka 1990 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2007, ikijinasibu kuwa ina lenga kuimarisha afya za wananchi wote, na kipaumbele kinatolewa kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuugua, ambayo ni watoto chini ya umri wa miaka mitano na wajawazito.

Marekebisho ya Sera ya Afya yanalenga pia kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kuwa karibu na wananchi, kwa kujenga zahanati kwa kila kijiji, pamoja na vituo vya afya kwa kila kata, ili kuwaondolea adha wananchi kufuata huduma za matibabu umbali mrefu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ng'wamadelanha, Manyambo Joseph, anasema kutokana na kijiji hicho kutokuwa na zahanati, wajawazito, wanaumia zaidi, wakibebwa na mikokoteni.

Anasema kijiji hicho pia kinakabiliwa na ubovu na ukosefu wa barabara, ambapo hata gari la wagonjwa haliwezi kupita, na wamekuwa wakiwabeba wajawazito kwenye mikokoteni ya ng'ombe kuwafikisha Shilabela.

"Hapa kijijini tuna ujenzi wa zahanati ambayo ipo kwenye hatua za ukamilishaji, na itakapoanza kufanya kazi itakuwa mkombozi wetu na kuondokana na adha ya kuwabeba wajawazito kwenye mikokoteni ya ng'ombe,"anasema Joseph.

### KUJIFUNGULIA NYUMBANI

Lega Kulwa ni mwanamama wa kijiji hicho cha Ng'wamadelanha, anayesema ukosefu wa zahanati kijijini humo, unasababisha wanawake wengi kujifungulia nyumbani sehemu ambayo siyo salama, na endapo wakizidiwa au kupata matatizo wanakwenda hospitalini.

Mwanamama mwingine Matha George, anasema wajawazito katika kijiji hicho hawaendi hata kliniki kujua maendeleo ya watoto wao na hali za ujauzito, pamoja na kupata elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, kutokana na umbali unaowachosha kwenye kufuata matibabu.

"Huduma za matibabu zinapokuwa umbali mrefu wenye kuteseka ni wanawake na watoto, hivyo tunaiomba serikali itukamilishie zahanati kwenye kijiji chetu, ili tuondokane na changamoto ya kubebwa kwenye mikokoteni kwenda kujifungua,"anasema Matha.

"Tunavyobebwa kwenye mikokoteni ya ng'ombe, au kubebwa kwenye bodaboda kutokana na huduma kuwa mbali, tuna jifungulia njiani," anaongeza.

Mwanamama mwingine Florensia Faustine, anasema wajawazito wanapojifungulia nyumbani maisha yao na watoto huwa hatarini, kutokana na ukosefu wa vifaa maalum vya kuzalishia, utaalamu, kupoteza damu nyingi na wakati mwingine watoto hunywa maji ya uzazi na kupoteza maisha.

Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza Deogratius Mashamba, anasema baada ya wananchi wa kijiji hicho cha Ng'wamadelanha kupata changamoto ya huduma za afya kuwa mbali, walikubaliana kujenga zahanati.

Anasema walianza kujenga kwa kutoa nguvu zao na kisha serikali kuanza kuikamilisha na sasa ipo hatua za mwisho.

Anasema ujenzi huo una zaidi ya miaka 10 na matarajio ya serikali ni kuikamilisha mwaka huu na kuanza kufanya kazi, ili kuondoa adha ya wananchi kufuata huduma za matibabu umbali mrefu, kuepusha mateso na vifo vya wajawazito na watoto vitokanavyo na uzazi, ambavyo vingezuilika.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Kamati ulinzi mwanamke, mtoto ziingie kazini kustawisha jamii

MIKOA mbalimbali inakabiliana na ongezeko la vitendo vya ukatili wa kijinsia, hali inayodhihirisha kuwa kazi ya kupambana na matendo hayo inahitaji juhudi zaidi.

Vita yake ni endelevu kutokana na ukweli kuwa vitendo vya kikatili vinazorotesha juhudi za kufikia maendeleo kuanzia ngazi ya familia, jamii na taifa pia.

Kundi la wanawake na watoto ni muhimu katika juhudi za kujenga ustawi bora wa jamii na kufikia nchi yenye maendeleo katika nyanja za kisiasa, uongozi, jamii na uchumi.

Pamoja na umuhimu wa kundi hilo hasa wanawake ambao kitaifa ni asilimia zaidi ya 50 ya idadi ya Watanzania, katika ustawi wa jamii na maendeleo, baadhi ya wanajamii wanashiriki kulifanyia ukatili hali inayoathiri juhudi zinazofanyika za kufikia ustawi na maendeleo.

Februari mwaka huu jijini Dodoma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anatoa rai kwa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zinazotekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kuweka mikakati ya kupambana na vitendo vya ukatili vinavyotokea sehemu mbalimbali.

Uundwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ni juhudi zinazofanywa na serikali katika mapambano ya vitendo vya kikatili kama vile ubakaji, ukeketaji, ulawiti, kuwapiga wanawake, ajira za watoto na mimba za utotoni kutokana na umuhimu wa kujenga jamii yenye amani, furaha na ustawi, serikali haina budi kushirikiana na asasi za kiraia, viongozi wa dini na jamii kufanikisha vita dhidi ya vitendo vya kikatili.



Ukatili dhidi ya watoto na utumikishwaji haramu ni masuala ya kudhibitiwa na kamati za MTAKUWWA. **PICHA MTANDAO**

> “Vitendo vya ukatili haviwezi kupungua kama kamati za ulinzi wa wanawake na watoto hazitasimama imara katika mapambano haya.

Utendaji kazi usioridhisha wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto hususani kwenye ngazi za serikali za mitaa na vijiji unatajwa kuwa miongoni mwa changamoto zinazoathiri mapambano ya ukatili wa kijinsia.

Kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zilizoko kwenye mitaa na vijiji ni nguzo muhimu katika utoaji wa taarifa za vitendo vya ukatili kwani ndizo kamati zinazoishi na wanajamii moja kwa moja. Kwa hiyo, ufanisi wa utendaji kazi wa kamati hizo utasaidia hatua madhubuti kuchukuliwa dhidi ya wote wanaoshiriki katika vitendo vya ukatili wa wanawake na watoto.

Ongezeko la vitendo vya ukatili katika jamii, limesababisha kuongezeka idadi ya kamati za ulinzi wa wanawake na watoto ili kukabiliana na unyanyasaji huo.

“Kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 18,186 zimeanzishwa katika ngazi ya taifa, mkoa, halmashauri, kata, vijiji na mitaa, mwaka 2021 ikilinganishwa na kamati 16,343 mwaka 2019 sawa na ongezeko la kamati 1843,” anasema Dk. Dorothy.

Ongezeko la kamati za ulinzi ni jambo moja lakini ufanisi katika utendaji ni jambo la msingi zaidi kufanikisha vita ya ukatili wa kijinsia.

Kwa hiyo, kamati zote kuanzia ngazi ya taifa hadi mitaa zinapaswa kuingia katika utendaji kazi ili malengo ya kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022 yafikiwe.

Ni vyema kamati hizi zitekeleze kikamilifu wajibu wao ili kusaidia kujenga jamii yenye furaha, amani na ustawi bora kwa maendeleo endelevu.

Vitendo vya ukatili haviwezi kupungua kama kamati za ulinzi wa wanawake na watoto hazitasimama imara katika mapambano haya.

Muda wa kamati hizi kukaa maofisi kusubiri taarifa za ukatili umepitwa na wakati, badala yake wanawajibika kufuatilia na kuchukua hatua dhidi ya ukatili.

Vilevile, kamati hizi zizingatie kuwa mwaka huu 2022 unapaswa kuwa mwaka wa mafanikio katika mapambano ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ikizingatiwa kuwa malengo ni kupunguza ukatili kwa asilimia 50 ndani ya mwaka huu.

Mafanikio ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto yanachagiza kufikiwa kwa mipango ya maendeleo katika nchi yetu kutokana na umuhimu wa kundi hili katika jamii.

Wasichana ambao ni mama na wazazi wa baadaye, wakipata haki ya elimu bila ubaguzi, watajikomboa kifikra na kiuchumi na hatimaye taifa kupata maendeleo.

Ni jukumu la kamati za ulinzi wa wanawake na watoto nchi kushirikiana na jamii ili kupata taarifa muhimu zitakazowezesha kuwa na mawasiliano na hatimaye kuchukuliwa hatua dhidi ya wahusika wa vitendo vya ukatili.

Halikadhalika, jamii inawajibika kuwafichua wahusika wa vitendo vya ukatili ili hatua stahiki badala ya kuendelea kuoneana aibu.

Watanzania wana wajibu wa kuifanya ajenda ya mapambano ya vitendo vya ukatili kuwa ya kitaifa ili kila mtu aone anawajibika katika kuchangia mafanikio na ustawi wa jamii kwa kuondoa vitendo vya kikatili. Tutafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari Mlali ya Kongwa, Dodoma.***

***Maoni:*** 0620-800462.

## Safari ya wajawazito kubebwa na ng’ombe kwenda zahanati

**INATOKA UK.11**

Diwani wa Pandagichiza, Charles Kabogo, anasema kwenye kata hiyo kuna vijiji vya Sayu, Pandagichiza, Ng’wamadelanha na Shilabela, ambavyo vyote vinategemea zahanati hiyo moja, lakini kijiji hicho cha Ng’wamadelanha ndicho kilichoko mbali zaidi ya vijiji vyote.

Anasema vijiji hivyo vingine ambavyo havina zahanati vipo katika hatua ya ujenzi, na kwamba zahanati ya kijiji cha Ng’wamadelanha awali, kijiji kilipokea Sh. milioni 50 kwa ajili ya kuikamilisha, na sasa wamepokea tena milioni 20 fedha za mapato ya ndani ya halmashauri, na wanajenga vyoo vya nje na ndani, pamoja na shimo la kutupa taka za uzazi.

“Ukosefu wa zahanati kwa kila kijiji ni tatizo kubwa kwa wananchi kupata huduma za matibabu hasa kwa wajawazito, ndiyo maana maeneo mengi ya vijijini kujifungulia nyumbani, na endapo mjamzito akipata matatizo wakati wa kujifungua kuna uwezekano mkubwa wa kupoteza maisha,”anasema Kabogo.

Mganga Mkuu wa Zahanati ya Shilabela wilayani Shinyanga, Nassoro Ahmed, anasema wamekuwa wakipokea wagonjwa wengi, na wakati mwingine wanaelemewa kutokana na uchache wa wauguzi kwenye akisema wapo watatu, na kwa siku moja hutoa matibabu kwa wagonjwa zaidi ya 30 hadi 40.

Anasema wakifunga si kwamba wanapumzika wanaendelea kutoa huduma za dharura kwa wajawazito na wagonjwa wa dharura zikiwamo pia ajali.

ELIMU

NA SHABAN NJIA,
SHINYANGA

# Bila cheti cha kuzaliwa hakuna ndoa

## • Ulinzi mkali magulioni na mnadani

UKATILI wa kijinsia kwa watoto na wanawake unaweza kuelezwa kama kaa la moto licha ya juhudi za serikali na wadau kupambana kulipunguza kwenye jamii.

Mathalani unyanyasaji umekuwa ukifanyika kutokana na tamaa za mali za baadhi ya wazazi wanaowaozesha watoto katika umri mdogo, ili kupata pesa au mifugo.

Ripoti ya Jeshi la Polisi ya hivi karibuni inaonyesha ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili wa kijinsia kwa kinamama na watoto kwa mwaka 2020 visa 7,388 vikiripotiwa kote nchini tofauti na mwaka 2015, matukio yalikuwa 5,803.

Jeshi la Polisi linakuja na ripoti hiyo katika kipindi hicho ambacho wazazi na walezi wengi wanatajwa kutokuwa karibu na watoto wao, wengi wakijihusisha na kusaka maisha bora ili kuzipa mahitaji ya msingi familia zao.

Pia miongoni mwa ukatili dhidi ya watoto ulioripotiwa kwa kiwango kikubwa kuwa kunyanyaswa kingono.

Mwaka 2020 kuliripotiwa visa 7,263 ikiwa ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwaka 2015 ambao vilirikodiwa visa 5,803, hii ikiwa ni sawa na matukio 615 kwa mwezi jambo ambalo linahatarisha mustakabali wa ustawi kwa watoto nchini.

Takwimu za Wizaya ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Makundi Maalum za mwaka 2017 pekee, zinasema zaidi ya matukio 40,000 ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo na akinamama yameripotiwa na watetezi wa masuala ya haki za watoto. Yanayotajwa kuwa chanzo ni imani za kishirikina na utandawazi kuwa miongoni mwa sababu za kuongezeka kwa matukio hayo.

Kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo, Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT) unashirikiana na asasi za kirai, Jeshi la Polisi (madawati ya jinsia), Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga pamoja na Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Shinyanga (SPC) katika kukabiliana na matukio ya ukatili huo.

Mradi unaanza na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga katika kata 26, na huko mashirika ya Thubutu Afrika Intiatives, WEADO, Rafiki SDO, Yawe, Green Community Intiatives (GCI), Agape na Radio Faraja, wameanza kazi Januari mwaka huu na kuendelea hadi Machi.

Glory Mbia, Mwakilishi wa WFT anasema, mradi wa ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake unalenga kupunguza vitendo vya kikatili ndani ya familia na jamii unafanyakazi na hadi sasa Shilingi milioni 170 zimetolewa kwa mashirika saba.



Ulinzi wa watoto ili wasome na kufikia hatima bora za maisha yao ni muhimu kwa maendeleo endelevu. **PICHA: MTANDAO**

> Matarajio yetu kwenye utekelezaji wa mradi huu, ni kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii, kupunguza ama kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Anawataja wahusika kuwa ni dawati la jinsia, klabu ya SPC, Radio Faraja na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, kila mmoja akipangiwa eneo la kufanyia kazi.

"Matarajio yetu kwenye utekelezaji wa mradi huu, ni kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii, kupunguza ama kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto," anasema Mbia.

### ULINZI MNADANI

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Puni, unapotekelezwa mradi huo, Fumbuka Mathias, anasema, wamekubaliana na wananchi wa kata hiyo kuwasindikiza watoto katika maeneo ya minada na magulio ili kuwalinda dhidi ya wahalifu wanaoweza kuwafanyia vitendo vya kikatili ikiwamo ubakaji na ulawiti.

Anasema, lengo la kuweka makubaliano hayo ni kuhakikisha watoto wa kike wanasoma na kuhitimu masomo katika hali ya usalama kwani wamebaini siku za magulio na minada ndipo yanapokwenda kufanyika matendo maovu dhidi ya watoto hao.

Kadhalika anasema, wamepitisha sheria ndogo za vijiji na mojawapo ni kuzuia sheria ya ndoa yoyote itakayofungwa katika vijiji vyao bila uongozi wa serikali za vijiji na ofisi ya mtendaji wa kata kufahamu ili kwa kuona cheti za kuzaliwa ili kujiridhisha kuwa wanaoona wana umri unaotajwa kisheria na siyo watoto wa chini ya miaka 18.

Mwananchi kutoka kata ya Puni Hamisi Masanja, anasema, uwepo wa makubaliano hayo umefanikisha kupunguza ukatili wa kijinsia kwa watoto, kwani hakuna vitendo vya ubakaji na ulawiti tofauti ilivyokuwa hapo awali.

Anasema kabla ya kuingia makubaliano ya kuwasindika watoto magulioni, matukio hayo yalirindima.

### KUTUMIA VYETI

"Hivi karibu mtoto wangu alitaka kuoa wakati najianda kwenda kutoa mahari ili ndoa ifungwe, nikaamua kwenda kujiridhisha na wazee wenzangu kama muolewa ana umri ambao unaotajwa kisheria au lah. Nilishangaa."

Anasema cha kushangaa walikuta binti anayeolewa ana miaka 16 na ndoa haikufungwa.

Angelina Dohole, mzazi kutoka Puni anaongeza kuwa, ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo hasa wanafunzi ulikuwa unafanywa siku za magulio na minada baada ya kurubuniwa na vijana wanaokutana nao siku hizo, lakini kuwasindikiza kumepunguza matendo hayo.

### WAGANGA WAHUSISHWA

Damson Fofo, miongoni mwa wajumbe wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ya kata hiyo, anasema, awali kabla ya kuundwa kwa kamati hiyo kulikuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia na asilimia kubwa ya wahanga walikuwa ni kinamama na watoto.

Anasema watoto wa kike walipelekwa kwa waganga wa jadi kuogesha dawa za mvuto wa mapenzi na kwamba wazazi wengi walikuwa wakiyafanya hayo ili kuepukana na mimba za utoto au za kable ya kuolewa.

Walifanya hivyo kwa mabinti zao bila kutambua kumwozesha mtoto akiwa na umri wa chini ya miaka 18 ni ukatili, lakini anasema baada ya kuundwa kwa kamati hiyo na kuanza kutoa elimu ya ukatili matukio yamepungua.

Mjumbe mwingine Lucy Michael anasema, wamekuwa wakikutana kila baada ya miezi mitatu na kwa mwaka mmoja wanakutana mara nne lengo likiwa ni kukumbushana wajibu na kuendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa wananchi waliko pembezoni mwa kata ili watambue wapi wanatakiwa kuanza kutoa taarifa.

Lucy anaongeza kuwa siku ya magulio na minada wajumbe wamekuwa wakifika na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na kuwasihi wazazi kuongozana na watoto wao siku hizo ili wanaume au vijana wanawarubuni watoto wao hasa wanafunzi wasipate nafasi.

### UHABA SEKONDARI

Happynes Kishimba ni mzazi anayeshughulikia tatizo hilo, akisema ukosefu wa sekondari katika kata ya Puni, umesababisha baadhi ya wanafunzi hasa wa kike kuacha masomo na kubaki majumbani baada ya kutembea umbali wa kilometa 10 kwenda shuleni na kurudi nyumbani kwenye Sekondari ya Itwangi iliyokoKata ya Nyida.

Anasema, Kata ya Puni haina sekondari na badala yake wanafunzi wanalazimika kutembea umbali mrefu kupata elimu hali ambayo imewalazimisha wazazi na walezi kutenga eneo la ekari 58 za ujenzi wa sekondari lakini, ujenzi bado haufanyiki na hakuna hatua zilizochukuliwa na serikali.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Maafa tabianchi yanavyoiweka Afrika kwenye kona mbaya



Athari za kimbunga cha Ana kilichotokea mwaka huu na kuathiri maisha na uchumi nchi za Madagascar, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe. Baada ya hapo kilifuatiwa na Batsirai kilichoiharibu zaidi Madagascar. **PICHA: MTANDAO**

> Mkutano huo wa COP27 utakaofanyika Misri eneo la Sharm-el-Sheik, huenda usiwe na tija kwa Afrika kama hakutakuwa na fedha za kuisaidia kukabiliana na matokeo ya athari za mabadiliko hayo.

JOPO la Umoja wa Mataifa la Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), linachambua na kuripoti taarifa za mabadiliko ya tabianchi huku, likizitaja nchi maskini kuwa zinakabiliwa na kitisho kikubwa cha mabadiliko hayo.

Kwa mfano mataifa yaliyo kwenye ukanda wa tropiki kama Afrika, Asia Kusini na Visiwa vya Pacific kuwa na hatari kubwa ya kukabiliwa na majanga na athari zaidi.

IPCC na Shirikisho la Hali ya Hewa Duniani (WMO) vinaeleza kuwa takwimu za maafa zilizotolewa mwaka jana zinaonyesha kuwa watu takribani bilioni 4.5 wameathirika na athari za mabadiliko ya tabianchi katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, lakini matatizo yakiwa makubwa zaidi miaka 20 iliyopita.

Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi hasa upande wa jirani na Madagascar ziko kwenye hati hati kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na hivi karibuni kimbunga cha Tropiki cha Batsirai kilipiga Madagascar na kusababisha athari mbaya.

Takriban watu 21,000 walikimbia makazi yao na nyumba 20,500 ziliharibiwa, kujaa mafuriko, au kuharibiwa.

Wakati jamii za watu zikiwa zinaamka au kupona kutokana na kimbunga Ana na Batsirai, taarifa za hali ya hewa za wiki hii zinaeleza kuwapo kwa kimbunga kingine cha Emnat ambacho mfumo wake unajiunda na kuanzia kwenye Bahari ya Hindi na Madagascar ni miongoni mwa waathirika.

Kimbunga hicho kinaelezwa kuwa kilikuwa na uwezekano wa kuipiga pwani ya Mashariki ya Madagascar pengine kuanzia kesho na kuelezea kitisho kingine kwa taifa hilo la Afrika ya Mashariki jirani na Msumbiji.

Shirika la Hali ya Hewa Duniani (IMO) linaeleza kuwa kimbunga cha Batsirai kimekuwa na athari kubwa kwa maisha kuanzia kuumiza uchumi, kilimo, makazi na ustawi wa watu.

Katibu Mkuu wa WMO, Petteri Taalas, akizungumza na jopo la wataalamu wa mabadiliko ya tabianchi anasema fikra kuwa ongezeko la nyuzi joto mbili sentigredi (2°C) lilikuwa jambo ambalo limebadilisha mawazo yaliyokuwapo hapo mwanzoni kuhusu changamoto za hali ya hewa duniani.

Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi maarufu COP2, uliofanyika mwezi Novemba mwaka jana nchini Scotland, haukuonyesha namna bora ya kuisaidia nchi maskini kama Afrika na Asia licha ya kuwa zinatajwa kuwa zitaathirika zaidi.

Kinachoikwamisha Afrika ni pamoja na kukosa rasilimali kama fedha, utaalamu na vitendea kazi hasa katika mazingira magumu ya kukabiliana athari mathalani kimbunga kama hicho kilichotokea Madagascar.

Kinachosumbua zaidi ni ahadi hewa za fedha zinazotolewa na mataifa yanayochangia kuchafua anga za juu kwa kuzalisha gesi au hewa ukaa kwa wingi au kwa mabilioni ya tani kila siku.

Mataifa hayo ni pamoja na Marekani, China na India. Katika mikutano ya COP mataifa tajiri viongozi wake wamekuwa wakieleza namna ambavyo watasaidia mataifa maskini lakini kwa ujumla hakuna kinachofanyika kwasababu hayatimizi ahadi.

Mkutano wa mabadiliko ya tabianchi COP27 mwaka huu unatarajiwa kufanyika Misri mwaka huu ukiwa umeletwa Afrika, lakini kazi kubwa itakuwa ni kuhakikisha fedha zinazoahidiwa zinatolewa vinginevyo itakuwa ni ubabaishaji.

Licha ya WMO kueleza kuwa mabadiliko ya tabianchi yana athari kwenye uchumi, chakula, miundombinu, hali za anga za juu na afya za binadamu kinachosisitizwa zaidi ni kuwa na mikakati ya uhimilivu na kuendelea na maisha (adapt strategies).

Ikimaanishwa kuwa watakaoathiriwa ni lazima wawe tayari kukabiliana na ukame, mafuriko, vimbunga, dhoruba, matukio ya jotokali, uhaba wa maji, upepo mkali na maeneo ya pwani kuzama baharini.

Mkutano huo wa COP27 utakaofanyika Misri eneo la Sharm-el-Sheik, huenda usiwe na tija kwa Afrika kama hakutakuwa na fedha za kuisaidia kukabiliana na matokeo ya athari za mabadiliko hayo.

Katibu Mkuu wa WMO, Petteri Taalas, akizungumzia mkutano wa Misri anasema "Tunaamini kutakuwa na upendeleo maalumu wa Afrika bara ambalo lipo kwenye hatari na hali mbaya zaidi," anaeleza.

Akizungumzia jinsi ya kuzisaidia Afrika na Visiwa vya Caribbean kuwa na uhimilivu na kuweza kutoka kwenye athari hizo (adaptation) Taalas anasema WMO inaelekeza nguvu kwenye kutoa taarifa za tahadhari na kuchukua hatua mapema (multi hazard early warning) zinazolenga kutambua na kuepuka athari mbaya za matukio yatakayotokea.

Anataja mkakati mpya wa kupata fedha kuwezesha kufanikisha upatikanaji wa huduma kama maji kwa watakaothrika, anasema shirika hilo litashirikiana na wadau kama Benki ya Dunia (WWB), Umoja wa Ulaya, UNDP, Shirika la Green Climate Fund, kupata fedha kwa ajili ya WMO kuwekeza kwenye kutoa taarifa za awali za tahadahari za maafa na namna bora ya kukabiliana nazo.

Changamoto za kukabiliana na athari za majanga Afrika ni kubwa na bila msaada wa kimataifa ni vigumu, kwa mfano hivi karibuni Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Misaada ya Dharura (OCHA), ilitangaza kutenga dola milioni 2.5 kusaidia maafa ya kimbunga cha batsirai kilichotokea Madagascar.

Mkuu wa OCHA Martin Griffiths, anaahidi kuwa fedha hizo zitapelekwa kwenye kutoa maji ya kunywa na chakula, huduma za afya kwa simu, kuhudumia wazazi, kusaidia waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia, vifaa vya makazi na bidhaa za msingi za nyumbani, kusaidizi wanafunzi shuleni.

Ni wazi kwamba bila usaidizi wa jumuiya kimataifa na kuzipa taasisi za kushughulikia maafa za nchi maskini fedha inakuwa vigumu kwa mataifa maskini kuhudumia watu wake kwenye majanga hasa hayo yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.



## Siku ya Maridhiano kuhamasisha sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, amesema kuwa Siku ya Maridhiano itafanyika kitaifa mkoani humo Machi 3, mwaka huu, huku shughuli mbalimbali zitafanyika ikiwamo kuhamasisha Watanzania kushiriki kwenye Sensa ya Watu na Makazi Agosti mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya siku hiyo, mwenyekiti huyo alisema wataelimisha na kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa kujiandikisha kwenye zoezi la sensa ya watu na makazi ambayo itakayofanyika mwaka huu.

"Serikali yetu mnafahamu inahitaji kuwafikishia watu wake maendeleo, lakini bila kujua idadi yake bado itakuwa ni tatizo, hivyo jumuiya inatumia nafasi hii kwenye kipindi hiki tunachoelekea kufanyika kwa maadhimisho hayo ya 'Maridhiano Day' viongozi watawaelimisha pia watu wetu umuhimu wa kujitokeza kujiandikisha kwenye zoezi hilo la kujiandikisha kwenye sensa ya watu na makazi,"alifafanua.

Pia alisema kutakuwa na uchangiaji damu utafanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma ili kusaidia wenye uhitaji.

"Jumuiya hii itakuwa imeisaidia serikali katika kuongeza upatikanaji wa damu kutokana na hivi sasa una uhitaji mkubwa wa damu ili kusaidia jamii ambayo haina uwezo pindi wanapotakiwa kuwekewa."

"Shughuli zingine zitakazofanyika kwenye kuelekea maadhimisho haya katika maeneo mengine ya Mkoa ni pamoja na upandaji miti sehemu mbalimbali zikiwamo za kitaasisi kama vile shule, nyumba za ibada dini, majumbani na katika ofisi za kiserikali," alisema.

Aisema wataiunga serikali kwa kuhimiza upandaji miti ili mazingira yawe ya kijani na kurudisha uoto wa asili uliotoweka.

Dk. Chande alisema kuwa kwenye maadhimisho hayo kwa upande wa nyumba za ibada zitaendelea kufanya maombi kwa ajili ya kuiombea nchi na viongozi.

# Elimu kwa watoto wa kike yahimizwa

**Renatha Msungu,** CHEMBA

WAZAZI katika Wilaya ya Chemba, wametakiwa kuwapa hamasa ya kusoma watoto wao wa kike ili wafikie ndoto zao.

Ofisa Elimu Taaluma (Sekondari) wilayani humo, Hausi Mkwachu, aliyasema hayo jana kwenye uzinduzi wa uhamasishaji kuondoa vikwazo ili mtoto wa kike apate elimu bora, ambao unatekelezwa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) na Woman Wake Up (WOWAP).

Alisema watoto wa kike hasa wa maeneo ya pembezoni wamekuwa wakikabiliana na vikwazo vingi kwenye njia zao, hivyo wazazi wanapaswa kuwa karibu na watoto ili kuwapa hamasa ya kutokata tamaa.

"Katika fursa mtoto wa kike anakabiliana na vikwazo ukilinganisha na mtoto wa kiume, hususani katika jamii zetu za kiafrika, hivyo tunapaswa kuliangalia hilo na kuwasaidia watoto wa kike ili watimize ndoto zao," alisema Mkwachu.

Aliongeza: "Miaka ya nyuma kulikuwa na wanafunzi wengi wanaoacha shule kutokana na sababu mbalimbali, ilifikia asilimia nne hadi tano, ambapo baada ya kufanya jitihada za makusudi kwa kutumia viongozi wa kijamii, wanaokatisha masomo sasa ni asilimia 1.9."

Mkwachu alisema hivi sasa wilaya hiyo imepiga hatua kubwa katika ufaulu ikiwa ni juhudi za serikali na wadau mbalimbali wa elimu ambapo ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 34 kwa mwaka 2018 na kufikia asilimia 78.8 mwaka 2021.

Kwa upande wake, Meneja Miradi wa TEN/MET, Alistidia Kamugisha, alisema kwa mwaka 2020 waliona ni vyema kufanya wiki ya elimu na kuweka msukumo wa elimu katika Wilaya ya Chemba kutokana na kutofanya vizuri kwenye mtihani wa darasa la saba.

"Tuliingia Chemba kupitia juma la elimu ndio maana tumekuja kutambulisha mradi wa uhamasishaji wa kuondoa vikwazo ili mtoto wa kike apate elimu bora," alisema Kamugisha.

Alisema mradi huo utashirikisha shule sita, ikiwamo tatu za msingi na tatu za sekondari, ambapo za msingi ni Kelema, Soya na Mrijo huku za Sekondari ni Mrijo, Soya na kwa Mtoro.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Godfrey Kasekenya (wapili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Dodoma, Mhandisi John Temu, wakati akikagua kazi iliyofanywa na wakala huo ya ufungaji wa daraja la chuma katika Mto Bubuku, wilayani Chemba, mkoani Dodoma juzi, baada ya la zamani kukatika na kusimamisha shughuli za usafirishaji katika eneo hilo. **PICHA: WUU**

# Utendaji wa WCF wamkosha Waziri Katambi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amesema Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo ni mfano wa kuigwa kutokana na utendaji wake katika kuihudumia jamii.

Katambi alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo kwenye hafla ya kukabidhi kompyuta kwa Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma zilizotolewa na WCF kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema WCF inafanya vizuri katika kazi zake hadi kutoa misaada kwa serikali, hivyo inastahili kupongezwa kutokana na kuonyesha mfano huo hapa nchini.

"Mfuko huu umekuwa ukitekeleza majukumu yake kisasa zaidi hivyo mifuko mingine inatakiwa kuiga mfano huu mzuri wa WCF katika kuwahudumia wateja wake na kutoa misaada serikalini," alisema.

Alipongeza mfuko huo kwa kuwekeza kwenye ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuanzia usajili, kupokea michango hadi kuchakata madai vyote kwa njia ya mtandao.

Kadhalika, alisema kuwa WCF imefanikiwa kulipa mabilioni ya fidia kwa kipindi kifupi sana tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, hivyo kupunguza malalamiko kwenye jamii.

Pia alisema serikali iliona umuhimu wa kuboresha mazingira ya uwekezaji ndio maana iliridhia punguzo la michango ya wafanyakazi kwa waajiri wa sekta binafsi kutoka asilimia moja hadi 0.6 pamoja na punguzo la tozo kutoka asilimia kumi hadi asilimia mbili.

Alibainisha kwa lengo la punguzo hilo ni kuweka mazingira rafiki zaidi ya uwekezaji hapa nchini, na hiyo ndio dira ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, alisema Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma ina wajibu mkubwa kuhakikisha wananchi wanapokea huduma zilizokusudiwa kwa kusimamia vyema nidhamu ya watumishi wa umma.

"Napongeza WCF kwa kuandaa machapisho yenye miongozo mbalimbali kuhusu fidia kwa wafanyakazi kwa nukta nundu ambayo yalikabidhiwa kwa Jumuiya ya Watu Wasioona (TAB) wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Maandishi ya Nukta Nundu(Braille) pamoja na misaada ya fimbo nyeupe kwa jamii hiyo yenye mahitaji maalum," alisema.

Naye Katibu Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma, Mathew Kirama, alishukuru kwa msaada waliotoa kwao utasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema kwa kutambua umuhimu wa mahitaji ya ofisi hiyo, WCF iliona ishiriki katika kusaidia upatikanaji wa kompyuta za mezani kwa lengo la kuongeza ufanisi kwenye majukumu yao.



# Juma Homera ataka elimu vijijini ya CHF

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kuhamasisha wakazi wa Mkoa wa Mbeya kujiunga na Mfuko wa Bima ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa, Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, amesema elimu kwa waishio vijijini bado inahitajika kwa sababu mwamko bado ni mdogo.

Alisema licha ya Halmashauri na Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa, lakini mwamko wa waishio vijijini kujiunga na mfuko huo bado ni mdogo na kuwaomba wataalamu wa afya kuyafikia maeneo hayo.

Alifafanua kuwa kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Busokelo inaendelea na zoezi la uhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa ambapo hadi kufikia Januari 2022 jumla ya kaya 1,879 kati ya kaya 24,187.

"Wilaya ya Chunya jumla ya kaya 3,743 kati ya 33,573 zenye wanachama 18,102 sawa na asilimia 11.4 huku Kyela ikifikia wastani wa 5.9 ya lengo kwa kuandikisha kaya 3,180, lakini inaendelea kuhamasisha kupitia mikutano ya hadhara kwa kuwatumia maofisa wanane kuwatembelea wananchi," alisema Homera.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imefanikiwa kuandikisha kaya 4,225 zenye jumla ya wanafamilia 15,898 zoezi hilo likihusisha vijiji vyote 152 kuhamasisha kujiunga na CHF iliyoboreshwa.

Katika hatua nyingine, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, alisema licha ya kuwahamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa, lakini wanaendelea kuwahimiza kuchangia shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Alisema katika kuhakikisha utekelezaji wa wananchi kushiriki ujenzi wa vituo vya afya kwa Wilaya ya Kyela walitoa nguvu kazi ya usombaji tofali, uchimbaji msingi, kumwaga zege la jamvi na lenta, kusogeza mawe na mchanga ambapo nguvu kazi hiyo inathamani ya shilingi milioni 12.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Lahmeyer Consulting Engineers Ltd, Mhandisi Ngwisa Mpembe (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Mbeya, CPA Gilbert Kayange, wakibadilishana nyaraka baada ya kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji wa Mto Kiwira, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Miradi ya Mbarali sasa kutekelezwa kwa bil. 38.7/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya Mbarali, imedhamiria kukusanya Sh. bilioni 38 .7 kutoka vyanzo mbalimbali kwa lengo la kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbarali, Twalib Lubandamo, alisema licha ya kuweka makisio ya Sh. bilioni 38.7 bado wameweka baki ya mwaka 2020/2021 kiasi cha Sh. milioni 747 na kufanya jumla ya mapato yote kuwa Sh. bilioni 39.4.

Alifafanua kuwa kwa Septemba 2021 halmashauri ilikusanya jumla ya Sh. bilioni tatu kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya halmashauri ikiwa ni sawa na asilimia 106 ya lengo la mwezi la Sh. bilioni tatu na kufikisha jumla ya mapato bilioni tisa yaliyokusanywa hadi sasa ikiwa ni asilimia 24 ya lengo la mwaka.

"Kwa mapato ya ndani, halmashauri ilikusanya Sh. milioni 445 kwa Septemba 2021 ikiwa ni asilimia 108 ya lengo la mwezi la Sh. milioni 411 na kufikisha jumla ya mapato ya bilioni moja yaliyokusanywa hadi sasa ikiwa ni asilimia 34 ya lengo la mwaka bilioni nne," alisema Lubandamo.

Kwa kuzingatia bajeti hiyo halmashauri imepanga kuboresha stendi ya mabasi ya Rujewa ili kuzuia maji kutuama kwa kuzingatia ukarabati wa choo.

Alisema miongoni mwa miradi itayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya pamoja na miundombinu ya barabara na madaraja.

Kwa upande wake, Diwani Bahati Salum, alisema halmashauri imetenga Sh. milioni 10 kwa ajili ya maboresho ya ukarabati wa Zahanati ya Imalilo Songwe ili kusaidia upatikanaji wa maji, ujenzi wa vyoo pamoja na upanuzi wa chumba cha kujifungulia.

**"Kwa mapato ya ndani, halmashauri ilikusanya Sh. milioni 445 kwa Septemba 2021 ikiwa ni asilimia 108 ya lengo la mwezi la Sh. milioni 411 na kufikisha jumla ya mapato ya bilioni moja yaliyokusanywa hadi sasa ikiwa ni asilimia 34 ya lengo la mwaka bilioni nne," alisema Lubandamo.**

## Wachimbaji wadogo wa dhahabu watakiwa kujiunga kwenye vikundi

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MBUNGE wa Lupa wilayani Chunya, Masache Kasaka, amehamasisha wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu migodini kujiunga kwenye vikundi ili waweze kupata mikopo ya asilimia 10 na kuanzisha miradi mingine ya kiuchumi.

Masache alitoa kauli hiyo juzi ambapo alisema vijana wanaojishughulisha na uchimbaji madini ya dhahabu wanapaswa kujiunga kwenye vikundi ili kupata sifa ya kukopesheka.

Alisema kilio kikubwa cha vijana hao ni mikopo ili kuongeza mitaji kwenye shughuli za uchimbaji madini pamoja na kubuni shughuli nyingine.

"Nawaomba wananchi hususani vijana ambao shughuli zao za uchimbaji wa madini, vibarua na biashara zingine wajiunge kwenye vikundi fedha zipo kwenye halmashauri na ni sera ambayo inaelekeza mikopo asilimia 10 zielekezwe huko ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu," alisema Kasaka. Aidha, alisema kuwa akiwa kama mwakilishi wao amejipanga kuhakikisha vijana wanakuwa na miradi ya kiuchumi mbali na kazi kwenye migodi na hata kujihusisha na uchimbaji mdogo wa madini.

"Sera inaelekeza vijana, wanawake na wenye ulemavu wapate mikopo hivyo ni wakati wao sasa kuchangamkia fursa hiyo," alisema.

Mchimbaji wa Kata ya Matundasi, Emmanuel Jackson, alisema kuwa shughuli za uchimbaji wa madini zinahitaki mtaji mkubwa, hivyo wanaiomba serikali kuwapatia mikopo ya vifaa vya kisasa ili kwenda na wakati na si uchimbaji wa kubahatisha.

"Shughuli za madini hazihitaji fedha mkononi, hivyo tupatiwe mikopo ya vifaa vya utafutaji uchimbaji kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kuchana na kuchimba kwa mazoea," alisema Jackson.



# Anwani za makazi kukamilika Mei

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Muungano na Zanzibar, kwa pamoja zinashirikiana kutekeleza mfumo wa anwani za makazi nchini, kwenye mikoa yote ili kukamilika ifikapo Mei, kwa lengo la kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi, inayotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Akizungumza kwenye kikao cha utekelezaji wa mfumo huo Mjini Zanzibar, jana, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, aliwataka wakuu wa mikoa mitano ya Zanzibar, kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya mchakato huo, zinatumika kama zilivyo kusudiwa.

Hemed alisema serikali imetenga fedha Sh. bilioni 28 kwa mikoa yote ya Tanzania, kwa ajili ya zoezi hilo, hivyo serikali haitakuwa tayari kuona fedha hizo zikitumika kinyume na matarajio na kwamba, endapo fedha hizo zitatumika tofauti na matarajio, wakuu wa mikoa watapoteza nyadhifa zao.

"Nimeamua kulisema hili, ili zoezi hili kufanikiwa na fedha hizi zikitumika vyenginevyo nawaambia wakuu wa mikoa safari zenu zitaishia hapo, tutawaengua," alisema Hemed.

Aidha, aliwataka viongozi wa serikali kuwa wazalendo na kusimamia maslahi ya Taifa, akisema serikali zote mbili zimekusudia kutekeleza mfumo wa anwani za makazi ili kurahisisha utambuzi wa wakazi na kila mwananchi kupata makazi katika eneo lake analoishi.

Alisema mfumo huo wa makazi umethibitika ni mfumo bora unaoendana na mabadiliko ya teknolojia duniani, hasa katika kufanikisha uchumi wa kidigitali na manufaa yake ni kurahisisha masuala ya ulinzi na usalama, ikiwamo shughuli za zimamoto na uokoaji.

"Kukosekana kwa mfumo wa uhakika wa utambuzi wa wakazi na makazi kuna athari nyingi za kiuchumi, kiusalama na kijamii," alisema Hemed.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alisema kuwa utekelezaji wa mfumo huo, ni tofauti ila unategemeana na pia operesheni hiyo imelenga kuongeza nguvu mchakato wa sensa.

"Anwani za makazi ni safari ya kuelekea Tanzania ya kidijitali, bila anwani za makazi Tanzania ya kidijitali haiwezekani, tayari dunia imeshaenda kidijitali, sisi ni sehemu ya dunia kama tunataka kwenda kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda ni lazima tutekeleze mfumo wa anwani za makazi na Zanzibar ya kidijitali inawezekana," alisema Nape.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema masuala hayo yanahitaji ushirikiano wa pamoja hivyo baada ya kikao kila mmoja achukue jukumu lake la kuhakikisha anwani za makazi na sensa ya watu inakamilika ipasavyo.

"Ni lazima wananchi wajue kibao hiki kipo hapa kwa manufaa gani, hivyo ni muhimu kujenga uelewa kwa wananchi, ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kupatikana," alisisitiza waziri huyo.

## Marufuku ya muziki wa usiku yasisitizwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Muhammed, amesema agizo la serikali la kupiga marufuku shughuli za ngoma na muziki baada ya saa sita usiku, halijafutwa na lipo katika utekelezaji.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, Nassor Salum, aliyetaka kufahamu agizo hilo iwapo limefutwa.

Masoud alisema, Mkoa wa Mjini Magharibi, unalisimamia agizo hilo kupitia masheha, hivyo wanatakiwa kutoa taarifa ikiwa ndani ya shehia zao bado kuna hali kama hiyo.

Alisema serikali ya Mkoa wa Mjini, itaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa agizo hilo linasimamiwa kwa kuwakumbusha masheha, kuongeza jitihada katika kutekeleza agizo hilo la serikali.

Wakati huo huo, waziri huyo akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini Machano, Othman Said, aliyetaka kujua mkakati wa serikali wa kudumu katika kukabiliana na tatizo sugu la kuzurura kwa wanyama kama ng'ombe na punda.

Masoud, alibainisha kwamba jumla ya wanyama 17 walikamatwa na wafugaji saba, walitozwa faini.

**Alisema serikali ya Mkoa wa Mjini, itaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa agizo hilo linasimamiwa kwa kuwakumbusha masheha, kuongeza jitihada katika kutekeleza agizo hilo la serikali.**




Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Biashara, Maendeleo na Viwanda, Omar Said Shabani, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## mikakati yaja kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, amesema kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi zimeenea kote duniani. Hivyo hatua kadhaa zinachukuliwa na serikali ikiwamo udhibiti na uhimilivu wa athari hizo kwa upandaji wa mikoko na ujenzi wa kuta katika maeneo mbalimbali ya fukwe. Imesema mabadiliko hayo yamesababisha kuwapo matukio mbalimbali yanayotokana na mabadiliko tabianchi, ikiwamo tsunami, kimbunga, mafuriko, upepo mkali, uhaba wa mvua au mvua kubwa.

Alisema kutokana na hali hiyo, maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba nayo pia yanakabiliwa na athari zinazoambatana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwa pamoja na mmomonyoka wa fukwe ukanda wa bahari na kuingia kwa maji ya chumvi kutokana na kupanda kwa kina cha bahari.

Mkuya, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Prof. Omar Fakih, aliyetaka kufahamu serikali inachukua hatua gani, kuzuia uvamizi wa chumvi katika bonde la kilimo cha juu katika ukanda wa bahari ya Mashariki ya Pemba.

Alisema pia serikali inaendelea kuchukua hatua mbadala, akisema mwaka 2013, mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa jamii, ulitekelezwa katika maeneo ya Tovuni, Ukele, Kisiwa Panza na Tumbe, kwa upandaji wa mikoko na ujenzi wa kuta kuzuia maji chumvi katika maeneo ya kilimo.

Aidha, alifafanua kuhusu bonde la kilimo cha juu cha watu wa Mjananza Pemba, hatua tayari zinaendelea kuchukuliwa na jumla ya Sh. 234,701,710 zimepangwa kujenga tuta na ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwaka huu.

Mkuya, alisema ujenzi huo utasaidia kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) hivyo wananchi kuendelea na shughuli zao za kilimo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 365/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HUSSEIN HASSAN UPAMBA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA SARAH BERNARD MWAMBOLA**

TANGAZO

*(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowowte/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 mwezi 3 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa msimamizi wa mirathi hiyo

Zingatia:endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakani kukaguliwa

**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 2 mwaka 2022**

## KUPOTEA KWA PASSPORTI YA KUSAFIRIA



**KAREN BONIFACE EMMANUEL** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba TAE320039 iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi **UHAMIAJI-PCO, DAR ES SALAAM** mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**CONTROL NAMBA.9910832145742**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JUMA RAPHAEL MASUKA** Anatangaza kupotelewa na **PASIPOTI** ya kusafiria yenye namba AB518052 iliyotolewa tarehe **23/04/2012 PCO-DAR ES SALAAM.** Iliibiwa pamoja na begi maeneo ya Igomela siku ya tarege **07/01/2022.** Atakayeiona ataoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo jirani yake. **Taarifa ya Polisi. MAJ/RB/141/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MANAV P. SANGHVI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 786 AAF – TOYOTA LANDCRUISER. CHASSIS NO. HDJ810000849. ENGINE NO. IHD0002522. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: IRI/IRI/RB/71074/2022.**

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

ISAYA NELSON JULIUS ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI(NISSAN PATROL) mali ya THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY yenye namba za usajili SU 38377 Chassis namba: JNITCSY61Z0577251
Injini namba : TD42212456
Kadi Namba : 2903528
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/74212/2022.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO. 3 OF 2022**
**In the matter of the estate of the late**
**MERY FIDELISI MASSAWE of HAZINA within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ISDORA VENZESLAUSIS KISHINDILIO**

<u>GENERAL CITATION</u>

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28 Day of 2,2022

**Date at Dodoma this 4th Day of January,2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE – DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa wa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 17/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HENERICO wa MIPANGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA MARIETHA NYANG'HOMA**

TANGAZO

*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 02 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Zingatia; endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 21 Mwezi 02 Mwaka 2022.**

HAKIMU

## KUPOTEAKWA KADI YA GARI

AYUBU ATHUMANI FUNDI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA OPA yenye usajili namba T591 DBX CHASIS namba ZCT100026181, INJINI namba 12Z1558872. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: DAR/KTS/RB/68527/2022

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE**
**OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 20 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late DYNESS MWITANWA KALIMBA**

**By 1. ESTHER CLAVERY MAUTA**
**2. ……………………………..**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28 day of FEB..2022

**Dated at Morogoro this 18th day of FEB..2022**

………………………………
RESIDENT MAGISTRATE

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

# *Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mke adaiwa kumchoma kisu mume mara 140

**FLORIDA,** MAREKANI

MWANAMKE mmoja katika Jimbo la Florida, anashtakiwa kwa mauaji, baada ya polisi kumtuhumu kumdunga kisu mume wake zaidi ya mara 140.

Joan Burke, 61, ambaye anashikiliwa bila dhamana, alifika mbele ya hakimu wa Kaunti ya Palm Beach, Jumapili kupitia mkutano wa video.

Katika ripoti ya tukio, maofisa wa Polisi wa Palm Spring, walisema walifika kwa Burke jioni ya Februari 11, baada ya kupokea simu kutoka kwa mtu aliyejitambulisha kuwa mtoto wa mshukiwa.

Mpiga simu alisema alikuwa amefika nyumbani kutoka kazini na kugundua mwili wa babake wa kambo, Melvin Weller, 62, ukiwa umelala jikoni kwenye dimbwi la damu.

Alipoulizwa ikiwa kuna mtu mwingine yeyote nyumbani wakati huo, mpiga simu, hakujibu, alitulia kwa sekunde kadhaa kisha kusema mama yake Joan Burke alikuwapo, ripoti hiyo ilisema.

Maofisa walipofika, walimpata mwathiriwa kwenye dimbwi kubwa la damu, lililofunika zaidi ya nusu ya sakafu ya jikoni. Wachunguzi pia waliukuta ufagio na zana zingine za kusafisha karibu na mwili.

Polisi walisema mwathiriwa, ambaye alionekana kuwa amefariki, alikuwa na majeraha mengi ya kuchomwa kisu na majeraha kwenye mwili wake.

Maofisa waliona damu zilizotapakaa ukutani, kabati na kaunta za jikoni huku visu kadhaa kikiwamo cha nyama, vikipatikana kwenye sinki la jikoni.

Wakati wa ukaguzi wa nyumba hiyo, maofisa walimgundua Burke akiwa amelala kitandani chumbani, akiwa na fahamu lakini alinyamaza kimya. Alisafirishwa hadi hospitali ya karibu kwa uchunguzi.

Uchunguzi wa maiti ulionyesha kwamba, mwathiriwa alipata majeraha zaidi ya 140 ya kuchomwa na kuvunjika fuvu la kichwa, lililosababishwa na pigo la kichwa na kisu cha nyama, ripoti hiyo ilisema. **BBC**

# Akamatwa kwa madai ulaghai wa mapenzi

**Bhubaneshwar,** INDIA

POLISI katika Jimbo la Bhubaneshwar, wamemkamata mwanaume anayedaiwa kuwalaghai wanawake 17 kwa kujifanya daktari na wakati mwingine hata ofisa mkuu wa afya.

Ramesh Chandra Swain, mwenye umri wa miaka 66, alikamatwa Jumapili wiki hii, usiku, katika nyumba moja eneo la Khandagiri, Bhubaneswar.

Remesh anatuhumiwa kuoa kwa njia ya ulaghai wanawake 17 kutoka majimbo nane na kuwaibia pesa.

Mkuu wa Polisi wa jimbo hilo, Bhubaneshwar, aliiambia BBC kwamba huenda mwanaume huyo aliwalaghai wanawake wengine kando na wanawake hao 17.

"Tumepokea taarifa kuhusu wanawake watatu kati ya 17 baada ya kukamatwa kwa Ramesh."

Maofisa pia wanachunguza simu ya mkononi ya Remesh ili kujua kuhusu fedha zake.

**Hatimaye Jumapili tulipata taarifa kwamba alikuwa amefika Bhubaneshwar na tukamkamata usiku huo huo nyumbani kwake Khandagiri.**

Akitoa taarifa za namna Ramesh alivyokamatwa, kamanda huyo alisema: Tumekuwa tukimtafuta mtu huyu kwa siku kadhaa, tumechukua kila hatua kumkamata. Lakini aliishi Bhubaneswar hivyo kwa muda fulani haikuwezekana kumkamata.

"Hatimaye Jumapili tulipata taarifa kwamba alikuwa amefika Bhubaneshwar na tukamkamata usiku huo huo nyumbani kwake Khandagiri," alisema Umashankar Das, Gavana wa Mkoa.

Msako wa polisi wa Bhubaneswar, kumtafuta Ramesh ulirekodiwa na mmoja wa wanawake 17 aliowadanganya.

Mwanafunzi mmoja wa kike mjini Delhi, alikuwa mwathirika wa mwisho wa Ramesh.

Baada ya siku chache, Ramesh alifika Bhubaneswar na mke wake mpya, wakatulia jengo la ghorofa huko Khandagiri.

Mwanamke huyo aligundua kuwa Remesh alikuwa na mwanamke mwingine na akafungua malalamiko dhidi ya Remesh.

Alipogundua kuwa polisi walikuwa wanamtafuta, alibadilisha nambari yake ya simu na kukimbia, kwa mujibu wa polisi, mwanaume huyo alikuwa na mwanamke mwingine, Guwahati wakati huo.

Jinsi alivyokuwa akidanganya wanawake Ramesh, mkazi wa Patkura katika Wilaya ya Kendrapara ya Odisha, alioa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1982, mke wake wa kwanza alijifungua watoto watatu wa kiume, kati yao ni madaktari na wanaishi nje ya nchi.

Mwaka 2002, miaka 20 baada ya ndoa yake ya kwanza, alimsaliti mwanamke huko Jharkhand. **BBC**



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi (katikati), akiwa na mwenzake wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, baada ya kuwasili mjini Kinshasa, juzi. **PICHA: AFP**

# Rais Erdogan aimarisha uhusiano Afrika

**KINSHASA,** DRC

RAIS wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, anajizatiti kuimarisha uhusiano na bara la Afrika katika nyanja mbalimbali ikiwamo usalama na biashara, huku juzi akizuru Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Amewasili DRC kwa makubaliano kadhaa ikiwamo ya usalama na akialikwa na mwenyeji wake Rais Felix Tshisekedi.

Tschisekedi baada ya kukutana na kiongozi huyo, aliweka wazi kwamba makubaliano yao ni yenye ushindi kwa pande zote mbili za nchi.

Katika ziara iliyoitwa ya kihistoria DRC, Rais Erdogan alifuatana na ujumbe wa maofisa wa serikali yake, pamoja na wafanyabiashara.

Pamoja na masuala mengine Rais Tshisekedi, alisema DRC na Uturuki, zimefikia makubaliano ya manufaa kwa pande zote mbili, kujenga ushirikiano kuhusu masuala ya usalama, miundombinu, afya pamoja na uchukuzi.

Rais Tshisekedi aliongeza kwamba DRC imeomba msaada Uturuki katika mapambano ya muda mrefu dhidi ya makundi ya waasi katika eneo lenye mgogoro la Mashariki.

Ziara hiyo ya Erdogan barani Afrika, iliyoanza Februari 20 itakamilika Februari 23, mwaka huu, kwa kutembelea pia Senegal na Guinea Bissau.

Septemba, mwaka jana, Rais Tshisekedi alifanya ziara rasmi mjini Ankara, Uturuki, akiwa na ajenda ya kutafuta ushirikiano wa kiuchumi na nchi hiyo pia alikwenda Istanbul Desemba mwaka jana, kushiriki mkutano wa kilele kati ya Uturuki na Afrika.

Uhusiano kati ya nchi hizo, kwa kipindi cha miaka mingi unakua na kiwango cha uwekezaji wa Uturuki na DRC, umeendelea kuongezeka huku biashara pande zote ikiongezeka kufikia dola milioni 40. Uturuki inalenga kujiimarisha zaidi katika bara la Afrika. **DW**

# NGASSA ATOA SIRI NKANE KUVAA JEZI YAKE YANGA

Na Adam Fungamwango

HATIMAYE winga wa zamani wa Yanga, Simba, Azam na Timu ya Taifa, Taifa Stars, Mrisho Ngassa, amefunguka sababu ya kupigania mchezaji Denis Nkane apewe jezi yenye namba aliyokuwa anavaa (16).

**Ngassa amesema kuwa wakati akicheza soka, Nkane alikuwa mdogo, lakini kila anapokwenda kufanya mazoezi binafsi alikuwa akija kumshuhudia na kuanza kuiga vitu mbalimbali , ikiwamo uchezaji kutoka kwake.**

Alisema kumwombea jezi namba 16 kwa viongozi wa Yanga wala haikuwa kwa bahati mbaya, kwani Nkane akiwa mtaani alikuwa akivaa jezi yenye namba hiyo.

"Huyu kijana alikuwa ananikubali sana. Wakati nakaa Yombo miaka ya nyuma, na yeye alikuwa anakaa kule kule, nikienda kufanya mazoezi binafsi na yeye anakuja kunishuhudia, na mimi nikaanza kumzoea, nikaona anaanza kuiga vitu vingi kutoka kwangu, uchezaji na kila kitu, kikubwa zaidi akaanza pia kuvaa jezi namba 16 akiwa mtaani kwetu pale, japo siyo ya Yanga," alisema Ngassa ambaye alipambana kutaka mchezaji huyo kinda apewe jezi namba 16 na kufanikiwa.

Nkane alisajiliwa na Yanga kipindi cha dirisha dogo akitokea Biashara United.

"Wala watu wasidhani eti nimefanya hivyo kwa sababu gani, hapana mimi namfahamu na nilifurahi sana kusikia amejiunga na Yanga, ndiyo maana nikaomba apewe namba hiyo kwa sababu najua anaipenda tangu huko nyuma. Pia anaweza kuvaa viatu vyangu kwa sababu kila kitu nilichokuwa nafanya na yeye alikuwa anatamani akifanye.

"Alikuwa anafuatilia mpaka video zangu na kuzifanyia kazi, kwa hiyo sina mashaka naye, ingawa kwa sasa majeraha kidogo yamemfanya akae nje, lakini ni mchezaji mzuri hilo wala halina shaka," alisema.



Bondia Manganga Kulwa akimpa wakati mgumu Hamadi Furahisha kwenye pambajo la raundi nne uzani wa Feather Kg 57, hatua ya nusu fainali ya Champion wa Kitaa, lililofanyika Dar Live, Mbagala nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Fainali Championi wa Kitaa sasa Machi

Na Saada Akida

FAINALI ya shindano la ngumi la kumtafuta Bingwa wa Kitaa (Champion wa Kitaa), limesogezwa mbele kutoka Februari 27 hadi mwanzoni mwa Machi mwaka huu litakapofanyika katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu Mkuu wa Peaktime Media, Meja Selemani Semunyu, ambao ni waandaaji wa fainali hizo, alisema lengo la kusogezwa mbele ni kuwapa nafasi mabondia walioingia fainali kujipanga vizuri.

"Fainali tumesogeza mbele kwa wiki mbili zaidi badala ya Februari 27, hivyo itachezwa Machi mwanzoni ambapo tutapata Bingwa wa Kitaa," alisema Semunyu.

Alitaja mabondia ambao wametinga kucheza fainali hiyo kuwa ni Abdallah Muhumba ambaye amempiga Shabani Kimimbi katika uzito wa Kg 52 huku pambano hilo likitarajiwa kurejewa baada ya mashabiki kutoridhia matokeo ya majaji wawili kwa mmoja.

Bondia wengine ambao wametinga fainali ni Omary Salum aliyempiga Bakari Kitogo katika uzito wa Kg 51, Peter Toshi akishinda baada ya kumchakaza Salum Zahoro na Swahibu Ramadhani akimchakaza Antony Peter katika uzito wa Kg 59. Sebastian Deo amefanikiwa kutinga fainali kwa ushindi wa majaji wote watatu kwa kumpiga Enock Enock katika uzito wa Kg 72 na Said Uwezo akimpiga David Edward katika uzito wa Kg 67.

Mabondia wengine ni Mrisho Mzezele aliyemtembezea kichapo Sadiq Jumbe katika uzito wa Kg 52 na Maneno Osward akishinda dhidi ya Khalifan Okala katika uzito wa Kg 57 huku Kennedy Samuel akimchakaza Shabani Kaoneka katika uzito wa Kg 76.

Mwingine ni Hamadi Furahisha akimpiga Manganga Kulwa katika uzito wa Kg 57 kwenye raundi sita.

Kwa mujibu wa Semunyu, mabondi hao wataenda kusindikiza pambano la Twaha Kiduku dhidi ya Alex Kabangu kutoka DR Congo, pambano hilo likitarajiwa kupigwa Machi 26, mwaka huu mkoani Morogoro.

## Manara sasa balozi wa Hunter

Na Mwandishi Wetu

MDAU wa soka nchini, Haji Manara, ameteuliwa kuwa Balozi wa Pikipiki za Hunter zinazozalishwa na Kampuni ya Hero na kusambazwa na Sunbeam Auto Ltd, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa kwenye ofisi za kampuni hiyo, Manara alibainisha kuwa atatumia ubalozi wake huo katika kutoa elimu kwa waendesha bodaboda ili kuepuka ajali za barabarani.

Alisema imekuwa ni kawaida kwa waendesha bodaboda kuendesha usafiri huo bila ya kuvaa kofia ngumu za kuwakinga na madhara ya majeraha pindi ajali ikitokea huku akisisitiza kuwa katika kila kona ya nchi atakayokuwa akienda kufanya kazi ya ubalozi wake huo, atajikita pia katika kutoa elimu ya kuwasaidia waendesha bodaboda kujinga na ajali.

"Kwa hatua hii ya bodaboda za Hunter kutoa kofia ngumu yaani hizi 'helmet' mbili kwa kila bodaboda moja wanayouza kwa ajili ya dereva na abiria, ni nzuri na yenye kuonyesha nia ya dhati ya kuwanusuru dhidi ya majeraha, hivyo kwangu nikiwa balozi mbali na kuzitangaza nitatangaza umuhimu wa kutii sheria za usalama barabarani," alisema Manara.

Alisema bei za bodaboda za Hunter 100 CC, 125 CC na Hunter 150 CC zinazofanya kazi kwa kaulimbiu ya "Piga gia barabara ishangae" ikielezea ubora wa pikipiki hizo zinazopatikana nchi nzima kwa mawakala 27 huku ikiwa na bima hadi ya Sh. milioni tano na huduma ya ukarabati mara tatu za mwanzo.

Kampuni ya Hero MotoCorp inaongoza kwa kutengeneza na kuzalisha pikipiki zinazoongoza kwa ubora duniani ambapo kwa Hunter 100CC inauzwa kwa Sh. milioni 2.45, na Hunter 125CC- inayouzwa kwa Sh. milioni 2.50 huku Hunter 150CC ikiuzwa kwa Sh. millioni 2.90. Pamoja na hayo kuna fursa za mikopo kwa wanaohitaji.

"Vipuri vya pikipiki hizi vinapatikana kila kona ya nchi kwa ajili ya kuwawezesha wateja wetu kuwa na uhakika wa kufanya matengenezo na niwasihi Watanzania kununua na kutumia aina hizi za pikipiki, kwanza bei zake ni rafiki na matumizi yake ni poa zaidi," alisema Ofisa Operesheni Mkuu wa Sunbeam Auto Ltd, Vinaykant Chaturvedi.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL WAKOMAA NA MORATA

ARSENAL bado wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 29, ambaye yuko kwa mkopo Juventus akitokea Atletico Madrid. (***Clciomercato, via The Boot Room***)

### STERLING KUBAKISHWA CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka klabu hiyo kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27. (***Fabrizio Romano on Twitter***).

### HERRERA KUNG'OLEWA ATLETICO

KLABU ya Houston Dynamo imetoa ofa ya kumsajili kiungo wa kati wa Atletico Madrid na Mexico, Hector Herrera mwenye umri wa miaka 31. (***MLS***)

### VAZQUEZ KUONDOKA MADRID

MLINZI wa Real Madrid, Lucas Vazquez mwenye umri wa miaka 30, anataka kuondoka katika klabu hiyo kwenda kwingineko kutafuta nafasi ya kucheza soka katika kikosi cha kwanza ili aweze kuwa katika kikosi cha Hispania kitakachoshiriki Kombe la Dunia. (***El Nacional***)

### DEPAY AWINDWA ITALIA

KLABU tatu za Italia, Inter Milan, AC Milan na Juventus zote zinavutiwa na mshambuliaji wa Barcelona na Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28. (Sport)

### SPURS KWA DE VRIJ

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mlinzi wa Inter Milan na Uholanzi, Stefan de Vrij mwenye umri wa miaka 30. (***InterLive, via Star***).

### EVERTON YATEGA WATATU

EVERTON inaweza kujaribu kumsajili mmoja wa wachezaji watatu wa Chelsea wanaocheza kwa mkopo, Billy Gilmour, Conor Gallagher au Armando Broja msimu huu wa majira ya joto. (***Mail***)

### BERGWIJN ATAKIWA MILAN

WINGA wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24, anaivutia AC Milan. (***Calciomercato***)

### FLAMENGO KUMKOSA PEREIRA

UHAMISHO wa kiungo wa kati wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 26, kwenda Flamengo unaweza kushindikana, matokeo ambayo yataifanya Manchester United kupoteza mamilioni. (***Sport Witness,Via Mirror***)

### BIELSA AGEUKA BUBU LEEDS

KOCHA Marcelo Bielsa amekataa kuzungumzia mustakabali wake huku kukiwa na uvumi iwapo atasalia kuwa kocha mkuu wa Leeds kwa msimu mwingine.(***Independent***)




# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI AMSIFU AUBAMEYANG KWA HAT-TRICK BARCA IKIUA

●●● Amefunga mabao maisha yake yote, ilitarajiwa kwamba angefunga hapa hivi karibuni pia, nimefurahishwa naye...

**BARCELONA,** HISPANIA

XAVI na Sergio Busquets walimsifu Pierre-Emerick Aubameyang baada ya mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal kufunga mabao matatu 'hat-trick' katika ushindi wa 4-1 wa Barcelona dhidi ya Valencia, Jumapili. Mshambulizi huyo wa Gabon alipachika wavuni mabao mawili na moja la Frenki De Jong na kuwapa Barca uongozi wa 3-0 kuelekea mapumziko, kabla ya kukamilisha mabao yake matatu dakika za lala salama, baada ya Carlos Soler kurudisha bao moja kwa Valencia.

Bao la nne la Barcelona katika mchezo huo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga uliopigwa juzi, Jumapili, awali lilipewa Pedri, lakini baadaye alitambulika Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, ambaye aligusa kabla ya kuingia wavuni.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Aubameyang, ambaye alikuwa akianza kwenye LaLiga kwa mara ya kwanza, kufunga mabao mengi kwenye mchezo wa ligi tangu alipofunga hat-trick akiwa na Arsenal dhidi ya Leeds United miezi 12 iliyopita, na Xavi alifurahishwa na mchango wa mshambuliaji huyo.

**"Amefunga mabao maisha yake yote," alisema Xavi akimsifia Aubameyang baada ya mchezo huo.**

"Ilitarajiwa kwamba angefunga hapa hivi karibuni pia. Anakwenda vizuri sana (kutafuta) nafasi, amekomaa, ana akili sana.

"Nimefurahishwa naye. Malengo haya yatakuwa mazuri sana kwake."

Bao la ufunguzi la Aubameyang lilimfanya kuwa mchezaji wa nne pekee kufunga katika Ligi Kuu za Hispania, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa karne hii, baada ya Stevan Jovetic, Michy Batshuayi, na James Rodriguez, huku mshambuliaji huyo pia akiwa mchezaji wa kwanza wa Gabon kufunga kwenye LaLiga.

Nahodha wa Barca, Busquets, alizidisha sifa zake kwa mchezaji mwenzake huyo mpya.

"Anafanya kazi vizuri sana, alifika na kukosa dakika, lakini anazipata sasa. Ni mchezaji mzuri," Busquets alisema.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 961,

MECHI KALI
BIASHARA UNITED
VERSUS
AZAM
1 | 3.18
X | 2.70
2 | 2.41

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# UTD YAWEKA REKODI YA KUSHINDA MECHI 700



**MANCHESTER,** England


KLABU ya Manchester United imekuwa timu ya kwanza kushinda michezo 700 ya Ligi Kuu England baada ya ushindi wao wa kusisimua wa 4-2 dhidi ya Leeds United, Jumapili.

'Mashetani Wekundu' hao walipata bao lao la kwanza pale Elland Road lililofungwa na nahodha, Harry Maguire kabla ya Bruno Fernandes kuongeza la pili. Lakini Rodrigo na Raphinha walirejesha usawa kwa mabao ya haraka mapema katika kipindi cha pili.

Hata hivyo, Fred alifunga la tatu baada ya kuingia akitokea benchi kabla ya mchezaji mwenzake wa benchi Anthony Elanga kufunga bao la nne mwishoni mwa mchezo. Kwa jumla, klabu hiyo ya Old Trafford imeshinda mechi 90 mbele ya Chelsea, ambao wameshinda mechi (610), huku Arsenal wakifunga katika nafasi ya tatu kwa ushindi mara 609.

Nyota wa Man United, Ryan Giggs ameshinda michezo mingi zaidi kwenye kinyang'anyiro cha klabu hiyo, akishinda mechi 407 kati ya 632. Paul Scholes ni wa pili kwenye orodha hiyo, akiwa ameshinda mara 321.

Kati ya ushindi wao wa 700 kati ya huo, 399 wameupata Old Trafford huku viwanja vya ugenini ambapo wamepata ushindi mkubwa ni Villa Park (17) na Goodison Park (17).



# Arteta: Odegaard anafaa kuwa nahodha

**LONDON,** England

MARTIN Odegaard ana sifa zote za kumfanya kuwa nahodha wa Arsenal, kwa mujibu wa kocha, Mikel Arteta.

Arteta alisema Odegaard "ana sifa zote" za kazi hiyo huku akizingatia nani anafaa kuchukua kitambaa ambacho awali kilikuwa cha Pierre-Emerick Aubameyang.

Baada ya Aubameyang kuhamia Barcelona, Arteta bado hajateua nahodha mpya wa wakati wote wa klabu hiyo.

Kieran Tierney ni mwingine ambaye Arteta anaweza kumgeukia, huku beki wa zamani w
'Washikabunduki' hao, Mar
Keown akiwa amemwanga
beki huyo wa kushoto kama m
anayefaa.

Akiwa na umri wa miaka 
Odegaard tayari ni nahod
wa Norway, na Arteta anaam
kuwa nafasi kama hiyo kati
ngazi ya klabu ingemfaa mchez
huyo wa zamani wa Real Madri

"Hakika ana sifa zote za kufa
ya hivyo," alisema Arteta.

"Anaonyesha kuwa na nidhan
na kiongozi mzuri uwanjani, 
ninaamini siku moja atafaa ku
nahodha wa Arsenal."

# ,840,460

# JACKPOT MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/02/22 | 18:00 | Brighton vs Aston Villa | 2.32 | 3.25 | 3.10 |
| 02. 26/02/22 | 18:00 | Brentford vs Newcastle | 2.41 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 26/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Hull City | 2.54 | 3.12 | 2.73 |
| 04. 26/02/22 | 18:00 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 05. 26/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Huddersfield | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 26/02/22 | 19:00 | Sivasspor vs Besiktas | 2.56 | 3.05 | 2.81 |
| 07. 26/02/22 | 20:30 | Oostende vs St Truiden | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 08. 26/02/22 | 22:45 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.75 | 3.44 | 2.47 |
| 09. 27/02/22 | 14:15 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 10. 27/02/22 | 15:30 | Hamburger SV vs Werder Bremen | 2.43 | 3.44 | 2.65 |
| 11. 27/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 12. 27/02/22 | 17:00 | Angers vs Lens | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 13. 27/02/22 | 17:00 | Metz vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 22/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4186 | Biashara United vs Azam | 3.18 | 2.70 | 2.41 |
| 16:05 | 1944 | AL Akhdood vs AL Nahdha | 2.16 | 2.98 | 3.31 |
| 17:30 | 4428 | Jeddah Club vs AL Sahel SC | 2.51 | 2.90 | 2.80 |
| 18:30 | 2212 | Alshoulla vs AL Kawkab | 2.04 | 2.94 | 3.72 |
| 18:30 | 5218 | Enppi Club vs El Ittihad Alexandria | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 19:00 | 2773 | Pardubice vs Slovacko | 4.29 | 3.84 | 1.77 |
| 20:00 | 1993 | Latina vs Avellino | 3.55 | 3.05 | 2.23 |
| 20:00 | 2945 | Olympiakos Nicosia vs Paeek | 1.48 | 4.05 | 6.72 |
| 20:00 | 5298 | Basaksehir vs Konyaspor | 2.18 | 3.20 | 3.30 |
| 20:30 | 1216 | Pisa vs Parma | 2.17 | 3.18 | 3.28 |
| 20:30 | 1979 | Spal vs Ternana | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 20:30 | 2262 | Alessandria vs Perugia | 2.85 | 2.90 | 2.60 |
| 20:30 | 2897 | Cremonese vs Vicenza | 1.60 | 3.66 | 5.47 |
| 20:30 | 3281 | Pordenone vs Monza | 3.79 | 3.30 | 1.95 |
| 21:00 | 1708 | Al Ahly Cairo vs Misr Lel Makasa | 1.15 | 6.72 | 18.77 |
| 21:30 | 3265 | FC Schaffhausen vs FC Thun | 1.77 | 3.66 | 3.81 |
| 22:45 | 1023 | Colchester vs Hartlepool | 2.44 | 3.14 | 2.84 |
| 22:45 | 1157 | Shrewsbury vs Portsmouth | 2.65 | 3.14 | 2.60 |
| 22:45 | 1297 | Cliftonville Belfast vs Warrenpoint | 1.18 | 5.96 | 11.54 |
| 22:45 | 1362 | Bradford City vs Harrogate | 2.18 | 3.24 | 3.19 |
| 22:45 | 1751 | Sunderland vs Burton | 1.71 | 3.68 | 4.51 |
| 22:45 | 1873 | Chesterfield vs Wrexham | 2.28 | 3.27 | 2.93 |
| 22:45 | 1883 | Solihull Moors vs Wealdstone | 1.47 | 4.30 | 5.87 |
| 22:45 | 1891 | Middlesbrough vs West Bromwich | 2.23 | 3.24 | 3.09 |
| 22:45 | 2028 | Wycombe vs Wigan | 2.76 | 3.20 | 2.46 |
| 22:45 | 2056 | Dagenham and Redbridge vs Woking | 1.82 | 3.57 | 3.91 |
| 22:45 | 2230 | Swindon Town vs Walsall | 1.96 | 3.39 | 3.63 |
| 22:45 | 2300 | Bristol City vs Coventry | 2.76 | 3.30 | 2.41 |
| 22:45 | 2632 | Fleetwood Town vs Sheffield Wed | 3.38 | 3.28 | 2.09 |
| 22:45 | 3046 | Gillingham vs AFC Wimbledon | 2.44 | 3.25 | 2.76 |
| 22:45 | 3407 | Cambridge Utd vs Plymouth | 2.98 | 3.32 | 2.26 |
| 22:45 | 3558 | Rochdale vs Port Vale | 2.29 | 3.29 | 2.94 |
| 22:45 | 3706 | Hull City vs Barnsley | 1.90 | 3.34 | 3.92 |
| 22:45 | 3773 | Leyton Orient vs Bristol Rovers | 2.26 | 3.23 | 3.04 |
| 22:45 | 3920 | Ipswich vs Cheltenham | 1.69 | 3.68 | 4.62 |
| 22:45 | 4287 | Falkirk FC vs Peterhead | 1.77 | 3.56 | 4.20 |
| 22:45 | 4299 | Notts County vs Halifax | 2.06 | 3.41 | 3.27 |
| 22:45 | 4926 | Scunthorpe vs Northampton | 3.77 | 3.33 | 1.94 |
| 22:45 | 4956 | Doncaster vs Accrington | 3.49 | 3.39 | 2.01 |
| 22:45 | 5107 | Rotherham vs Morecambe | 1.35 | 4.53 | 8.47 |
| 22:45 | 5397 | Crewe vs Oxford Utd | 3.82 | 3.53 | 1.87 |
| 22:45 | 5491 | Swansea vs Bournemouth | 2.99 | 3.24 | 2.29 |
| 22:45 | 5543 | Partick Thisle vs Morton | 1.68 | 3.63 | 4.70 |
| 22:45 | 5640 | Kelty Hearts FC vs Cowdenbeath | 1.23 | 5.40 | 9.63 |
| 22:45 | 5661 | Charlton vs MK Dons | 2.60 | 3.29 | 2.55 |
| 22:45 | 5858 | Preston vs Nottingham | 2.70 | 3.09 | 2.60 |
| 23:00 | 1348 | Bolton vs Lincoln | 1.97 | 3.44 | 3.54 |
| 23:00 | 2849 | Chelsea vs Lille | 1.32 | 5.20 | 9.01 |
| 23:00 | 5318 | Reading vs Birmingham | 2.61 | 3.25 | 2.56 |
| 23:00 | 5961 | Villarreal vs Juventus | 2.50 | 3.16 | 2.91 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MAYELE, KAGERE WAZIDI KUPIGWA PINI YA MABAO

Na Adam Fungamwango

BAO la dakika ya 38 lililofungwa na straika wa Geita Gold, anayekuja juu nchini kwa sasa, George Mpole wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu mjini Geita, limemfanya kufikisha mabao saba.

**Kwa idadi hiyo Mpole sasa anamzidi bao moja straika wa Yanga, Mkongomani Fiston Mayele mwenye mabao sita, lakini akimzidi kinara wa mabao kwa upande wa Simba, Meddie Kagere ambaye amesalia na mabao yake matano.**

Mpole, ambaye kwa sasa amekuwa hashikiki, akifunga mabao kwenye Ligi na Kombe la FA, anakamata nafasi ya pili kwenye orodha ya vinara wa ufungaji bora wa Ligi Kuu, akiwa amebakisha mabao mawili kumfikia kinara wa mabao kwa sasa Reliants Lusajo, ambaye ana mabao tisa mpaka sasa.

Ni msimu unaoonekana kuwa mzuri kwa mastraika wa Tanzania ambao wanaonekana kuongozana kwa wingi kwenye mbio za kusaka Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu Bara.

Hata hivyo, wakati Mpole na Lusajo wakifunga angalau bao moja kila baada ya mechi mbili au tatu kwa sasa, kuna wachezaji ambao ni kama wamepigwa breki au wamewekewa gundi miguuni kwani kwa muda mrefu wamesalia na mabao hayo hayo bila kuongeza.

Hao ni Jeremiah Juma wa Tanzania Prisons, Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania, ambao kila mmoja amesimama na mabao yake matano, lakini Kagere anayeonekana msimu huu kuwa na ukame wa kupachika mabao.

Wakati Lusajo ana mabao tisa, Mpole saba, Mayanga na Mayele wakiwa na sita, Kagere na Jeremiah wakiwa na matano, wachezaji Richardson Ng'ondya na Juma Luzio wa Mbeya City, Daniel Lyanga wa Geita Gold na Feisal Salum wa Yanga, wote wana mabao manne kila mmoja.



# Ushindi wa Ruvu maalum kwa Sonso

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Ruvu Shooting imesema ushindi wa bao 1-0 ilioupata juzi dhidi ya Tanzania Prisons ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, ni maalum kwa ajili ya mchezaji wao, Ally Mtoni Sonso (pichani) aliyefariki hivi karibuni jijini Dar es Salaam na kuzikwa katika makaburi ya Ndugumbi, Magomeni Makuti.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Mkwasa, amesema ilikuwa mechi ngumu, lakini vijana wake walipambana kuhakikisha wanashinda kwa ajili ya kumuenzi mchezaji mwenzao Sonso, ambaye amewaachia wachezaji wenzake majonzi makubwa.

"Mechi ilikuwa ngumu, tulikuwa tunacheza na timu ambayo tunapigania nayo nafasi moja, kipindi cha kwanza tuliwamiliki, lakini cha pili walitumia zaidi mipira mirefu, pia kulikuwa na utelezi, kwa hiyo ilituathiri sana. Tumefurahi kupata ushindi kwa sababu mechi ya kwanza tulipoteza kwa idadi kubwa ya mabao dhidi ya Simba kwenye Kombe la FA, na kwa kiasi kikubwa ilitokana na wachezaji wengi hawakuwa sawa kwa sababu ya kufiwa.

"Hivi nikwambie tu, kuna mchezaji alikuwa analala naye chumba kimoja, hadi leo hayupo sawa, na hajaanza kufanya mazoezi. Kwa ushindi huu nadhani wachezaji sasa kisaikolojia watakaa sawa, na ushindi huu wameupeleka kwa mwenzao aliyetangulia mbele za haki," alisema Mkwasa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire, alimtaja mchezaji ambaye hayuko vizuri mpaka sasa kuwa ni Saadat Mohamed.

"Huyu ndiye alikuwa anakaa na Sonso chumba kimoja, ameumia sana, amelia sana, alizimia na kupelekwa hospitali, hadi leo bado hajarejea kwenye hali ya kawaida, hii ni kuonyesha msiba ule ulivyotuathiri," alisema.

Bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa na Hamadi Majimengi na kuipeleka timu hiyo hadi nafasi ya 14, ikicheza mechi 15 na kujikusanyia pointi 15.



Michezo
Jumanne Februari 22, 2022
Nipashe



Xavi amsifu Aubameyang kwa hat-trick

UKURASA 21

BADO BERKANE...



Winga wa Simba, Bernard Morrison akishangilia sambamba na John Bocco baada ya nyota huyo raia wa Ghana kuifungia timu yake bao la kusawazisha dhidi ya USGN katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa General Seyni Kountche, Niamey nchini Niger. Simba iliondoka nchini humo jana kuelekea Morocco tayari kwa mechi ijayo dhidi ya RS Berkane. **PICHA: SIMBA**

## Simba, Yanga kazi ipo FA

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, Simba watacheza dhidi ya Pamba FC ya Mwanza katika mchezo wa robo fainali ya michuano hiyo huku Yanga yenyewe ikipepetana na Geita Gold kwenye hatua hiyo inayotarajiwa kuchezwa Aprili 8 hadi 13, mwaka huu.

Katika droo iliyopangwa juzi makao makuu ya Ofisi za Azam Media ambao ni wadhamini wa michuano hiyo, Simba watakuwa wenyeji ikiwakaribisha Pamba FC katika Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam wakati Yanga wakishuka dimbani hapo kuwakaribisha Geita Gold FC, huku Azam FC yenyewe ikiialika Polisi Tanzania katika dimba la Azam Complex na Coastal Union wakiwa wenyeji wa Kagera Sugar Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili baada ya droo hiyo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema robo fainali itakuwa ya ushindani kwa sababu mara nyingi timu kubwa zinapocheza na zilizoko ligi ya chini kuhitaji kumdhalilisha mkubwa.

"Tunapokutana na timu kama hizi hutakiwi kuingia kichwa kichwa itakuathiri, tunatambua juu ya hizi timu itakuwa mechi ngumu sana na Simba imejipanga kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kucheza nusu fainali na tunahitaji kukutana na mnyonge wetu (Yanga) katika michuano hii," alisema Ahmed Ally.

Naye Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Thabiti Kandoro, alisema Geita ni timu nzuri na walikutana katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania na mechi kuwa ya ushindani mkubwa.

# Adebayor kuvunjiwa benki Simba, waifuata Berkane

**Na Waandishi Wetu**

## Viongozi wakiri ni kifaa, Pablo atoa sababu kuambulia sare kwa USGN, sasa kujichimbia Casablanca...

BAADA ya kulazimisha sare ugenini juzi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, jana saa 12:00 jioni kwa saa za Niger ambazo ni sawa na saa 2:00 usiku kwa Afrika Mashariki, wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba walikwea pipa juu kwa juu kuelekea nchini Morocco tayari kwa mchezo unaofuata dhidi ya RS Berkane.

**Simba juzi iliondoka na pointi moja baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Union Sportive Gendarmerie Nationale (USGN) hiyo ikiwa mechi yake ya pili na ya kwanza ugenini kwenye hatua ya makundi, hivyo kukaa kileleni mwa Kundi D ikiwa na alama nne kutokana na kushinda 3-1 katika mechi ya kwanza nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast ambayo juzi nayo ilitoa kipigo kama hicho ikiwa kwao dhidi ya RS Berkane.**

Katika mchezo wa juzi, winga wa Union Sportive Gendarmerie Nationale, Victorien Adebayor, ambaye alionyesha kiwango cha hali ya juu alihusishwa na kutua Msimbazi msimu ujao, mwenyewe akisema hawezi kukataa ofa hiyo kama itakuja.

Winga huyo raia wa Niger, alionyesha uwezo mkubwa kwenye mechi hiyo, akiwachachafya mabeki wa Simba, lakini alifunga mabao mawili katika mechi ya klabu yake dhidi ya RS Berkane wakati walipoteza kwa mabao 5-3.

"Simba ni timu kubwa Afrika na kila mara inafanya vizuri, ni fahari kuchezea timu kubwa kama hii, wachezaji wengi wangetamani kuichezea, hata mimi, ikitokea fursa siwezi kuiacha kama watanihitaji," alisema Adebayor alipohojiwa baada ya mechi hiyo kumalizika.

Alipoulizwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', mapokeo yake kuhusu kauli ya winga huyo, alisema atamshawishi Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji 'kuvunja benki' ili kumsajili Adebayor ambaye anaichezea USGN kwa mkopo.

"Nimemwona, ni mchezaji mzuri, nilishawahi kuongea na wakala wake huko nyuma, kwa bahati mbaya kwa sasa amesajiliwa nchini Denmark, hapa anacheza kwa mkopo. Lakini leo nimezungumza tena na wakala wake asubuhi na hata saa hizi mechi imeisha nimeongea naye tena, na nitaongea na rais wa klabu hii avunje benki kwa ajili ya kumpata mchezaji huyu asirudi Ulaya, kwa sababu ana uwezo mkubwa, ana nguvu na spidi na anajua kufunga. Huyu ni mchezaji wa kuichezea Simba, wala hawezi kurudi Ulaya," alisema Try Again.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameeleza kuridhishwa na sare iliyopatikana ugenini juzi, huku akidai imepatikana kwenye mazingira magumu kutokana na baadhi ya wachezaji wake kukabiliwa na changamoto za kiafya zilizochangiwa na hali ya hewa.

"Tulitaka kushinda mechi hii, kwa sababu ndiyo malengo yetu, lakini ilishindikana kwa sababu nyingi, kwanza ugumu wa usafiri, hatukuwa na muda wa kujiandaa, tuliangalia mikanda ya mechi zao haraka haraka na wala hatukuwa na muda wa kufanyia mazoezi uwanjani, badala yake tuliwaelekeza tu wachezaji jinsi gani ya kufanya. Nashukuru wachezaji wetu walifuata maelekezo. Kupata sare ugenini kwa hali kama hii ni jambo la kujivunia kwa sababu pia hali ya hewa ya joto na vumbi ililituathiri wakati wa mchezo, kupumua kwa wachezaji ilikuwa shida pia," alisema kocha huyo.

Yalikuwa ni mabao ya Wilfried Gbeuli dakika ya 12 na Bernard Morrison dakika ya 84 yaliyoifanya mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi kuisha kwa sare ya bao 1-1.

Katika hatua nyingine Meneja Habari wa Simba, Ahmed Ally, amesema kikosi hicho kilitarajiwa kuondoka jana saa 12:00 jioni kwa saa za Niger sawa na saa 2:00 usiku kwa Tanzania, ambapo kitapitia Uturuki kabla ya kutua Morocco tayari kwa mechi yao dhidi ya RS Berkane itakayopigwa Jumapili wiki hii.

Alisema wamelazimika kwenda mapema nchini humo kutokana na hali ya baridi kali iliyoko huko kwa sasa, hivyo kuwapa muda wachezaji wakuizoea na kupumzika ambapo wataweka kambi ya siku tano jijini Casablaca kabla ya kuielekea mjini Berkane kwa mchezo huo.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >